# Nipashe

Jumanne Agosti 9, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581032

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,019,301,493/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#





RIPOTI MAALUM-3

**Shule** yenye mazingira hatarishi kwa walimu...

UKURASA 4




**DESCHAMPS ANAAMINI POGBA ATACHEZA KOMBE LA DUNIA**

UKURASA 22

# KICHEKO WAKULIMA

• **Samia** aagiza fedha ruzuku zitoke kabla Agosti 15, ashusha bei... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alipotembelea banda la TARI katika maonesho ya Siku ya Wakulima 'Nanenane' Uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya jana. **PICHA: IKULU**


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**UWANJA MWAKANGALE RASMI KUWA WA MAONESHO NANENANE**

SERIKALI imetangaza rasmi eneo la Uwanja wa John Mwakangale jijini hapo kuwa maalumu la maonesho ya wakulima (Nanenane) kitaifa...

UKURASA WA 5

**KUMEKUCHA MRADI BWAWA LA NYERERE**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema kasi ya ujenzi wa mradi wa kimkakati wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius...

UKURASA WA 19


**LEO NI LEO UCHAGUZI MKUU KENYA**

LEO Wakenya wanapiga kura kuamua viongozi watakaowaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo katika ngazi ya kitaifa mpaka...




## TPDC: Kila mteja kufikiwa huduma gesi asilia nyumbani

UKURASA 3



## Ujerumani yaipa Tanzania bil. 23.7/- utatuzi migogoro wanyamapori

UKURASA 2


MICHEZO **AZAM YAWASILI KUIVAA ZESCO** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati), akisindikizwa baada ya kufungua mkutano wa Taasisi za Maendeleo ya Kifedha (DFIs) kwa Ukanda wa Afrika Mashariki kujadili masuala ya Viwango Endelevu Toleo la 2. Wanaomsindikiza ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy (kushoto) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Maendeleo Endelevu la Ulaya (EOSD), Arshad Rab (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kicheko wakulima, serikali yashusha bei ya mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetangaza neema kwa wakulima nchini kwa kushusha bei ya mbolea kwa zaidi ya nusu ya bei iliyokuwa ikiuzwa msimu wa kilimo uliopita baada ya kuzindua Mpango wa Ruzuku kwenye pembejeo hizo.

Rais Samia Suluhu Hassan alizindua mpango huo jana jijini hapo alipokuwa akifunga Maonesho ya Wakulima (Nanenane) ambayo kitaifa yalifanyika katika mkoa huo.

Alimwagiza Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuhakikisha anatoa fedha hizo za ruzuku kabla ya Agosti 15, mwaka huu ili wakulima waanze kujiandaa mapema na msimu ujao wa kilimo.

Alisema serikali iliamua kuweka ruzuku kwenye pembejeo hizo kwa sababu msimu uliopita lilitokea tatizo la uhaba wa mbolea nchini uliosababishwa na kushuka kwa uzalishaji wa bidhaa hiyo duniani kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo mlipuko wa virusi vya corona.

Rais Samia alisema tatizo hilo lilisababisha kupaa kwa bei ya pembejeo hiyo na hivyo wakulima wengi wakashindwa kumudu hali iliyoshusha matumizi ya mbolea hizo na kusababisha kushusha mavuno.

"Njia pekee ya kushusha bei ya mbolea nchini tuliyoibaini ni kuweka ruzuku, tuliamua kutafuta fedha na kuiweka kwenye pembejeo hizi, sasa niwaombe wakulima, zalisheni mazao kibiashara ili tupate chakula kwa wingi na ziada tuuze kwa majirani zetu," alisisitiza Rais Samia.

Aliwataka wakulima pia kujipanga kuondokana na utegemezi wa ruzuku na badala yake iundwe mifuko ya mbolea ambayo itakuwa inatumika kushusha bei ya pembejeo hizo zinapopaa.

Aliwataka wakulima wote nchini kujisajili kwenye mfumo wa usajili unaoendelea ili iwe rahisi kunufaika na ruzuku hiyo ya mbolea kwa maelezo kuwa wakulima watakaopata mbolea hiyo ya ruzuku ni waliosajiliwa pekee huku akisisitiza kuwa miaka ijayo serikali itatoa vitambulisho maalumu kwa wakulima ambavyo vitawasaidia kupata huduma mbalimbali za kilimo.

Katika hatua nyingine Rais Samia aliwataka vijana kuingia kwenye kilimo na kuzalisha kwa wingi akisisitiza kuwa wameandaliwa mazingira mazuri ikiwamo maeneo ya kulima pamoja na pembejeo.

Akitoa taarifa ya bei mpya ya mbolea Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema kwa msimu ujao wa kilimo mbolea itakayouzwa kwa bei ya juu zaidi itauzwa Sh. 70,000 na ya chini zaidi itauzwa Sh. 50,000.

Waziri Bashe alisema msimu uliopita wa kilimo mbolea ya kupandia aina ya DAP ilikuwa inauzwa kwa wastani wa Sh. 131,675, lakini baada ya serikali kuweka ruzuku itauzwa Sh. 70,000, UREA ilikuwa inauzwa kwa zaidi ya Sh. 124,000, kwa sasa itauzwa Sh.70,000 pamoja na mbolea za NPK ambazo zilikuwa zinauzwa kwa zaidi ya Sh. 122,695 ambazo pia zitauzwa Sh. 70,000.

Vilevile, alisema mbolea ya SA iliyokuwa inauzwa kwa zaidi ya Sh. 82,000 sasa itauzwa Sh. 50,000 na CAN ambayo ilikuwa inauzwa kwa Sh.108,000 sasa hivi itauzwa kwa Sh. 60,000.

"Ruzuku hii tumeiwekea mfumo maalumu ambao utasaidia kuwanufaisha wakulima waliosajiliwa pekee, kila mfuko utakuwa na namba yake tofauti na mfuko mwingine, mkulima akishanunua mbolea hii atachukuliwa alama za vidole na tutapata taarifa moja kwa moja," alisema Bashe.

Wakulima watakaokuwa hawajajisajili, alisema wakienda kununua mbolea hizo watalazimika kujisajili kwanza kwa utaratibu maalumu na kwamba serikali ilipata uzoefu miaka ya nyuma ambayo ruzuku hiyo iliwahi kutolewa na ikawanufaisha wachache.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema mikoa hiyo kwa msimu uliopita ilizalisha mazao ya chakula kwa zaidi ya tani milioni 10 huku mahitaji yake ikiwa ni tani 5,000,000.

Aliomba serikali kuendelea kuyaweka maonyesho hayo katika mkoa huo, akisema kuwa ukanda huo ndiyo kinara wa uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara.

Aidha, katika maonesho hayo, Rais Samia alishuhudia utiliaji saini wa mikataba 21 ya kilimo cha umwagiliaji yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 180.

## Ujerumani yaipatia Tanzania msaada bil. 23.7/- utatuzi migororo wanyamapori

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI ya Ujerumani imeipatia Tanzania msaada wa Euro milioni 10 (Sh. bilioni 23.7) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitatu, ikiwamo utatuzi wa migogoro kati ya wanyamapori na binadamu wanaoishi pembezoni mwa hifadhi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana baada ya utiaji saini wa msaada huo, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alitaja miradi mingine ni upatikanaji wa haki za wanawake na watoto pamoja na uandaaji wa maandiko ya kitaalamu ya miradi.

Akielezea mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo, Tutuba alisema: "Euro milioni sita (Sh. bilioni 14.2) zitatumika kukabiliana na migongano kati ya wanyamapori na binadamu. Euro milioni tatu (Sh.bilioni 7.1) ni kwa ajili ya mradi wa kuwezesha upatikanaji wa haki za wanawake na watoto. Euro milioni moja (Sh. bilioni 2.3) ni kwa ajili ya kuandaa maandiko ya kitaalamu."

Tutuba alisema, mradi wa kukabiliana na migongano kati ya wanyamapori na binadamu utakuwa na lengo la kuhakikisha kwamba, serikali na mamlaka zinazojitegemea zinazosimamia maeneo tengefu, halmashauri zitakazochaguliwa na asasi za kijamii zinatekeleza kwa ufanisi mkakati wa Taifa wa kudhibiti migongano kati ya wanyamapori na binadamu.

Alisema, mradi huo pia utasaidia kuimarisha uwezo wa Tanzania kusimamia kwa ubora migongano kati ya wanyamapori na jamii zinazozunguka hifadhi za wanyamapori.

Tutuba alisema, hatua hiyo pia itamaliza vifo vinavyosababishwa na wanyamapori kwa jamii zinazozunguka baadhi ya hifadhi za wanyamapori na kuepusha uharibifu wa bayoanuai katika hifadhi za wanyamapori.

Alisema, mradi wa kuwezesha upatikanaji wa haki za wanawake na watoto utalenga upatikanaji wa haki kwa kundi hilo, kuwawezesha kisheria na kuwalinda na ubaguzi wa kijinsia na unyanyasaji ambako kutachochea kuongezeka kwa usawa wa kijinsia nchini.

Mradi huo pia utawezesha makundi maalumu hasa ya wanawake na wasichana kupata haki na ulinzi na kuwa na uwezo wa kudai haki zao, kupunguza unyanyasaji wa kijinsia.

"Msaada huu ni sehemu ya ahadi ya misaada ya Euro milioni 71 (Sh. bilioni 188.6) iliyoahidiwa na Ujerumani wakati wa majadiliano yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam, Novemba, mwaka jana kwa ajili ya miradi mbalimbali nchini," alisema Tutuba.

Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regine Hess, alisema msaada huo ni muhimu kwa maendeleo ya Tanzania, kwamba itasaidia kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo.

Alisema, mradi wa upatikanaji wa haki za watoto na wanawake utawezesha kuimarisha msaada wa kisheria na kuwalinda kutokana na ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia.

**HABARI KITAIFA**



Mafundi wakiendelea na utekelezaji wa mradi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP) lililoko Rufiji, ambalo linatarajiwa kutoa megawati 2,115 litakapokamilika, jana. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# TPDC: Kila mteja kufikiwa huduma gesi asilia nyumbani

**Na Jenifer Gilla**

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Nchini (TPDC), limesema mpango wa kuunganisha gesi asilia majumbani ni endelevu na linatarajia kila mteja kufikiwa na huduma hiyo.

Mikoa ambayo imeshafikiwa na huduma hiyo mpaka sasa ni Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani.

Mhandisi wa Mafuta kutoka TPDC, Aristides Katto, alisema lengo ni kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa ili kuwapa urahisi wa maisha.

"Kuna hii miradi ambayo inaendelea kukamilishwa kwa sasa maeneo ya Sinza na Kurasini ambapo mpaka tumeshaunganisha kaya 570.

"Pia tumeanza ushirikiano na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na miradi inayofuata itatekelezwa kupitia wao ambao maeneo tunayotegemea kuyafikia ni Mnazi Mmoja mkoani Lindi na Mkuranga," alisema.

Baadhi ya Watanzania waliounganishiwa gesi asilia majumbani na kulipa kulingana na matumizi, wamesema kuna nafuu kubwa kulinganisha ya gesi ya kununua kwenye mtungi.

Nipashe ilizungumza na baadhi ya wakazi jijini Dar es Salaam waliounganishiwa huduma hiyo na TPDC, Remis Mallya, mkazi Sinza alisema aliunganishiwa huduma hiyo Juni mwaka huu na ameona nafuu kubwa kwa kuwa analipa Sh. 30,000 kwa mwezi wakati awali akitumia mtungi wa kilo 13 kwa muda huo alikuwa akilipa Sh. 56,000.

"Tofauti ni kubwa ukilinganisha na gesi ya kwenye mitungi, kwa sababu gesi hii ya sasa nikilipia Sh. 1000 natumia kupikia siku nzima hadi kuchemshia maji ya kunywa, kwa maana hiyo kwa mwezi natumia Sh. 30,000 tu," alisema.

Nuru Makupula mkazi wa Mwenge, Mlalakuwa alisema kuwa anachofurahishwa kutoka kwenye huduma hiyo ni kununua gesi kulingana na uwezo wake na haina usumbufu wa kuifuata dukani.

Nuru mwenye familia ya watu 11, alisema kwa siku anatumia nusu uniti kwa gharama ya Sh. 500, sawa na Sh. 15,000 kwa mwezi tofauti na awali alilazimika kutumia mara tatu ya gharama hiyo.

"Kipindi hiki cha baridi ndiyo matumizi yanaongezeka kufikia uniti moja kwa siku kwa sababu tunachemshia watoto maji ya kuoga, lakini sijawahi kuvuka Sh. 1,000 kwa siku. Lakini pia nanunua kulingana na uwezo wangu, silazimishwi kutoa 50,000 kama ilivyo kwa gesi ya mtungi," alisema.

Agnes Shayo, mkazi wa Kawe alisema kuwa tangu amefungiwa gesi hiyo ameacha matumizi ya mkaa.

"Kwa mimi mwenye familia kubwa nilikuwa nalazimika kutumia mkaa kwa sababu gesi ilikuwa juu na inatumika mwezi mmoja tu, ila kwa sasa nimeacha mkaa, kwa sababu gesi hii gharama zake ni za chini sana, mimi sijawahi tumia zaidi ya Sh. 30,000 kwa mwezi na ninaitumia kupikia kila kitu," alisema.

Akizungumza na Radio One, mwishoni mwa wiki, Mhandisi wa TPDC, Eva Swilla, alisema gesi hiyo inapatikana kwa Sh. 1,000 kwa mita moja, gharama ambazo ni nafuu ikilinganishwa na gesi ya mitungi.

"Hii gesi ni asilia inatokea Mtwara na inafika kwenye nyumba ya mtu kwa njia ya mabomba kwa Sh. 1,000 kwa mita moja, ukija kulinganisha bei utakuta ni tofauti," alisema.

**UTUNZAJI MAZINGIRA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utu na Mazingira (HUDEFO), Sarah Pima, alisema kuwa mradi huo pamoja na kurahisisha ukali wa maisha, pia utapunguza uharibifu wa mazingira kwa ukataji miti kwa ajili ya kuni.

"Mimi hii gesi naiona kama ni mkombozi wa mazingira kwa sababu ikiwafikia Watanzania wengi wataachana na matumizi ya kuni na mkaa ambayo ndiyo sababu kuu ya ukataji wa miti kwa sasa. Hii gesi ya mitungi inayotumika majumbani kwa sasa haiwezi kutatua tatizo la kukatwa miti kwa sababu bado gharama zake ni za juu," alisema.

Mei mwaka huu, Waziri wa Nishati, January Makamba, akiwasilisha makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2022/23, alisema zimetengwa Sh. bilioni 10.00 kutekeleza mradi wa kupeleka na kusambaza gesi asilia kwenye makazi ya wananchi wanaoishi jirani na mkuza wa bomba kuu la gesi katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani.

Taarifa ya Benki ya Dunia (WB), inaeleza kuwa watu bilioni 2.8 duniani wanatumia teknolojia ya zamani kupikia, ambayo sio salama zinazogharimu dunia zaidi ya Dola trilioni 2.4 kila mwaka.

# Uwanja John Mwakangale rasmi kuwa wa maonesho Nanenane

**Na Renatha Msungu,** MBEYA

SERIKALI imetangaza rasmi eneo la Uwanja wa John Mwakangale jijini hapo kuwa maalumu la maonesho ya wakulima (Nanenane) kitaifa huku ikitangaza kuanza kujenga miundombinu ya kudumu kwa ajili ya shughuli hiyo.

Akizungumza wakati wa kufunga maonyesho ya kitaifa ya Nanenane, Waziri Bashe alisema viwanja vya John Mwakangale, vitaanza kufanyiwa marekebisho ili liwe eneo maalum la kitaifa kwa ajili ya maonesho hayo.

Alisema wameamua kufanya hivyo kutokana na mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuwa eneo la uzalishaji wa mazao mengi ya chakula na biashara nchini.

"Tutaanza ukarabati hivi karibuni lengo letu ni eneo hili kuwa bora kwa ajili ya maonesho haya kwa sababu ni makubwa," alisema Bashe.

Kuhusu eneo la Uyole ambalo wazee wa Mbeya wanatumika kulifanyia matambiko, alisema serikali imeliboresha kwa kulijengea uzio ambalo litawaruhusu wazee na wananchi kwa ujumla kuingia na kutoka kwa ajili ya kufanya ibada zao.

Hata hivyo, alisema kuna eneo ambalo serikali ilimelichukua kwa ajili ya shamba la kilimo na wakazi wa eneo hilo watalipwa fidia.

Kwa upande wake Waziri wa Fedha Dk. Mwigulu Nchemba, alizitaka taasisi za kilimo kuacha kuchekelea kuongezeka kwa bajeti ya kilimo pamoja na nyingine badala yake wakafanye kazi ili kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kwenye jitijada ya kuinua sekta ya kilimo.

Dk. Nchemba alisema serikali imewekeza bajeti kubwa kwenye sekta ya kilimo, taasisi na wananchi kwa ujumla wanapaswa kwenda kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha fedha ya bajeti iliyotolewa inatumika ipasavyo.

"Naomba mzingatie utendaji kazi kwenye sekta mbalimbali mjitume ili kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kilimo kinasonga mbele hapa nchini," alisema.

Kadhalika, alisema wataendelea kutekeleza maelekezo yote ambayo wametakiwa kufanya ili kuhakikisha kusudio la serikali linatimia kwenye sekta ya kilimo.

Alisema lengo lao ni kuona kila fedha ya serikali ilioekezwa kwenye miradi inatumika ipasavyo.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema watahakikisha wanawasimamia watumishi wa halmashauri waliopewa vifaa kwa ajili ya kusimamia sekta ya kilimo ili kuhakikisha wanavitumia kwa kazi hiyo.


## Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) Publication of Biannual Income and Expenditure

Lawyers' Environmental Action Team is, local Non-Governmental Organization which was found in 1994 and is registered under the NGOs Act of 2002 with (Certificate of Compliance No. 1985).

**Vision:** Tanzania with sustainable and well-managed environment and natural resources for current and future generations.

**Mission:** To contribute towards good governance in the use and sustainable management of the environment and natural resources through public interest litigation, advocacy, strategic research, capacity building, and networking.

In accordance with Non-Governmental Organization (Amendment) Regulation, 2018, Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) is pleased to publish the amount of funds received and expended from January 2022 to June 2022.

**Biannual Income and Expenditure for the period from January 2022 to June 2022**

**Income:**

| | | |
|---|---|---|
| Receipt from Donors | | 967,175,012.10 |
| Bank Interest | | 207,704.00 |
| **Total Income** | | **967,382,716.10** |
| **Expenditure on:** | | |
| Examining the Extractive Legal regime in Tanzania | | 27,997,421.82 |
| Usimamizi Endelevu wa Maliasili in Tanzania | | 855,730,630.62 |
| Collective Action for Rights Realization in the | | 83,654,663.66 |
| **Total Expenditure** | | **967,382,716.10** |

In sum, LEAT received grants from the following donors: Open Society Initiative for Eastern Africa

(OSIEA), United States Agency for International Development (USAID-Tanzania), and VSO-Tanzania.

**Lawyers' Environmental Action Team (LEAT),**
**Mazingira House, Mazingira Street,**
**Mikocheni B, P.O. Box 12605,**
**Dar es Salaam;**
**Email:** info @leat.or.tz.

21978901

RIPOTI MAALUM -3

## KIBORIANI

# Shule yenye mazingira hatarishi kwa wanafunzi, walimu na elimu

Na Sanula Athanas

**KATIKA sehemu ya pili jana, kulikuwa na ushuhuda wa wenyeji kuhusu madhila yanayowakabili wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi Kiboriani wilayani Mpwapwa. Endelea na sehemu ya tatu kujua shida zingine zilizoko shuleni hapo.**

---

**BARIDI LATAWALA SAKAFU**

Mwalimu wa Mazingira, Afya na Michezo shuleni hapo, Mussa Ahmad, ana malalamiko yake anayoyataja na kukiri ni mtihani mkubwa kwa walimu kufundisha na wanafunzi kujifunza, hivyo majumuisho yake ni kwamba hata lengo la taaluma shuleni hapo linakuwa njiapanda.

Anaanza kwa kutaja miundombinu duni ya madarasa inayowatesa wadau wote wa shughuli hiyo ya kitaaluma shuleni hapo, hasa asubuhi, akigusa wanafunzi wa darasa la awali hadi la pili wanaoketi sakafuni kwenye baridi kali ambalo si rahisi mtu kulihimili, pia walimu kushindwa kuingia darasani mapema asubuhi.

Hapo anasisitiza uzoefu wake namna yalivyo mazingira hasi kwa taaluma, akitaja baridi linawafanya wanafunzi kupata njaa zaidi.

Mwalimu Ahmad anaendelea: "Ule muda wa asubuhi unawaonea huruma wanafunzi, kunakuwa na baridi kali sana, mikono inakufa ngazi. Mbaya zaidi wanaketi kwenye sakafu ambapo pana baridi kali. Na mazingira haya ya baridi mtoto anakuwa na njaa sana, anapofika shuleni usomaji unakuwa mgumu mno.

"Kwa hiyo, ikifika saa nne asubuhi tunawaruhusu waende nyumbani kupata chakula walau kwa nusu saa. Mazingira ya darasani ni magumu sana, hususani wanafunzi wa madarasa ya chini (darasa la awali hadi la pili), darasani kunakuwa na baridi kali, yeye mwenyewe ameketi chini, sakafu inakuwa na baridi kali.

"Pia kunakuwa na ukungu unaoingia hadi ndani ya darasa, hivyo darasa nalo linakuwa na maji, hata ile hali ya mtoto kuandika inakuwa mbaya.

"Ule mvuke unapokuja darasani, unakuwa na vumbi lililochanganyika na maji, mtoto akiliweka daftari lake chini, linaloa, yeye mwenyewe mikono inakuwa imekufa ngazi, hata morali ya kujifunza inashuka.

"Mazingira haya pia siyo rafiki kwa walimu, wakati mwingine inafika saa mbili, saa tatu mwalimu anashindwa kuingia darasani kwa sababu kuna baridi kali sana.

"Kwa sasa hapa shuleni tupo walimu watano, kuna mwenzetu mmoja mwaka jana wakati anapanda mlima kuja huku kazini, alipata ajali ya pikipiki... Hadi leo ameshindwa kurejea kazini."

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule hiyo, Isaya Chitema, aliyekuwa mwanafunzi wa darasa la kwanza shuleni hapo miaka 40 iliyopita, anapalalamika kwa kauli: "Hapa ni bora elimu na siyo elimu bora. Serikali iboreshe mazingira ya shule hii."

Hata hivyo, Chitema (48) anaeleza hatua alizochukua kwa nafasi yake ni kwamba ameshawasilisha matatizo ya shule hiyo serikalini.




**"Ule muda wa asubuhi unawaonea huruma wanafunzi, kunakuwa na baridi kali sana, mikono inakufa ngazi."**

**HALI ILIVYO KITAALUMA**

Ufuatiliaji wa Nipashe kuhusu mwenendo wa kitaaluma wa Shule ya Msingi Kiboriani, umebaini shule hiyo si tu kwamba inafanya vibaya kiwilaya, bali pia kwa ngazi ya kitaifa.

Kwa mujibu wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), katika matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba mwaka 2020, Kiboriani iliyokuwa na watahiniwa 23, ilishika nafasi ya 44 kati ya shule 45 za Wilaya ya Mpwapwa zilizokuwa na watahimiwa chini ya 40. Kwa lugha rahisi, ilikuwa miongoni mwa shule mbili zilizofanya vibaya zaidi wilayani humo mwaka huo.

Kimkoa shule hiyo ilikamata nafasi ya 233 kati ya 261 na kitaifa ilikuwa ya 6,217 kati ya shule 6,641, ikiwa haina mtahiniwa aliyefaulu kwa daraja 'A', watatu walipata daraja 'B', wanane daraja 'C', 11 daraja 'D' na mmoja daraja 'E'.

| Jinsi | A | B | C | D | E |
|---|---|---|---|---|---|
| Wasichana | 0 | 2 | 4 | 6 | 1 |
| Wavulana | 0 | 1 | 4 | 5 | 0 |
| Jumla | 0 | 3 | 8 | 11 | 1 |

Mchanganuo wa matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba mwaka 2020 katika Shule ya Msingi Kiboriani. CHANZO: NECTA Agosti 2, 2022.

Tovuti rasmi ya NECTA pia inaonesha kuwa kwa mwaka uliofuata, yaani 2021, Shule ya Msingi Kiboriani iliyokuwa na watahimiwa 31 katika Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba, iliimarika kidogo, kiwilaya ikishika nafasi ya 34 kati ya shule 38 zilizokuwa na watahimiwa wasiozidi 40.

Kwa ngazi ya mkoa, ilishika nafasi ya 195 kati ya shule 221 na kitaifa ilikuwa ya 4,759 kati ya shule 5,664. Hiyo ina maana kwamba Kiboriani ilikuwa miongoni mwa shule tano za mwisho kiwilaya kwenye kundi lake na ya sita kutoka mkiani kwa ngazi ya mkoa.

Katika matokeo hayo ya mwaka 2021, hakuna mtahiniwa kutoka Kiboriani aliyefaulu kwa daraja 'A', mmoja alifaulu kwa daraja 'B', 17 walipata daraja 'C', 13 daraja 'D' na ina cha kujivunia kwa kutokuwa na mtahiniwa aliyefeli kwa alama za daraja 'E'.

| Jinsi | A | B | C | D | E |
|---|---|---|---|---|---|
| Wasichana | 0 | 1 | 7 | 11 | 0 |
| Wavulana | 0 | 0 | 10 | 2 | 0 |
| Jumla | 0 | 1 | 17 | 13 | 0 |

Mchanganuo wa matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba mwaka 2021 katika Shule ya Msingi Kiboriani. CHANZO: NECTA Agosti 2, 2022.

**MIKAKATI YA KIJIJI**

Safari ya Nipashe kijijini Kiboriani kupata undani wa kinachoisibu shule hiyo hata kuingia kwenye orodha ya shule za mwisho katika mitihani ya taifa wilayani Mpwapwa, ilihamia kwenye ofisi ya Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kiboriani, Ramadhan Mfundo.

Mbali na orodha ya madhila yanayoisibu Shule ya Msingi Kiboriani yanayotajwa na kila ngazi iliyohojiwa na Nipashe, Mfundo anaongeza angalizo lake la ziada.

Mfundo analia na historia mbaya kwa kijiji na shule yake kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi waliofaulu katika shule hiyo kuendelea na sekondari kwingineko, wengi wameishia njiani.

Anataja sababu kuu ni mwamko duni wa wazazi kuwasisitiza na kuwasimamia watoto wasonge mbele kimasomo, pia umbali wa kuzifikia shule za sekondari wanakodahiliwa.

Ofisa Mtendaji huyo ana orodha ya hatua kuu tatu wanazochukua kuinusuru shule, pia kupaisha elimu ambayo anakiri iko katika hali mbaya kijijini hapo.

Anataja kipaumbele cha kwanza ni kutatua tatizo kuu la vyoo shuleni, ambalo sasa kila familia ndani ya kijiji hicho chenye idadi ya watu 2,202 (kwa mujibu wa Sensa ya 2012) inachangia Sh. 5,000 na hadi Alhamisi ya wiki juzi, zilikuwa zimeshakusanywa Sh. milioni 1.239 zilizoko katika akaunti ya kijiji.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, kijiji hicho sasa kina familia takriban 440, hivyo kama kila familia itachangia Sh. 5,000, watakusanya jumla ya Sh. milioni 2.2 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa vyoo shuleni.

Mfundo anabainisha mikakati yao kwamba baada ya kukamilisha matundu ya choo, operesheni hiyo ya kupaisha elimu itahamia kwenye kujaza pengo la madawati, ambalo ni 85 kwa sasa ili kukidhi matakwa ya kisera.

Ofisa Mtendaji huyo pia anasema wameshaandika barua kwa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kuomba kupata kibali cha kukata miti kijijini hapo ili kutengeneza madawati, ombi ambalo Nipashe imethibitishiwa na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kwamba limekubaliwa.

Mfundo anataja hatua nyingine ambayo ni endelevu, inahusu kuleta mageuzi ya elimu kupitia kufanyika mikutano ya kila mara kuhamasisha elimu kijijini hapo.

***ITAENDELEA KESHO**

# Kumekucha mradi Bwawa la Nyerere

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema kasi ya ujenzi wa mradi wa kimkakati wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP), unaotarajiwa kutoa Megawati 2,115 imeongezeka kutokana na kubadilisha wasimamizi.

Kutokana na kasi hiyo ujenzi umefikia asilimia 67.18 hadi Julai mwaka huu kutoka asilimia 37, Juni mwaka 2021.

Vilevile, Waziri Makamba amesema ujazaji wa maji kwenye bwawa unakaribia kufanyika karibuni, huku Mhandisi Mkazi Lutengano Mwandambo, akibainisha kuwa bwawa hilo litajaa ndani ya misimu miwili ya mvua au mmoja kama itanyesha mvua kubwa.

Waziri Makamba alibainisha hayo jana wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi huo, baada ya kuwapo kwa minong'ono ya wananchi kuwa mradi huo hauendelei na utekelezwa.

Alisema uvumi huo unapaswa kupuuzwa huku akisisitiza mradi huo ni mkubwa utakaowaunganisha Watanzania na kwamba jitihada nyingi na za makusudi zinafanyika ili kuhakikisha unakamilika kwa viwango na ubora.

Alisema ukamilikaji wa mradi huo ni jambo moja na usambazaji wa umeme ni jingine, huku akisisitiza kuwa ubora na viwango ni jambo kubwa na muhimu zaidi katika utekelezaji wake.

"Mradi hausimami kwa sasa unaendeshwa asubuhi, mchana na usiku, Bodi katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), imebadilishwa ili kuimarisha usimamiaji na hii imesaidia kuongeza kasi ya mradi kwa kiasi kikubwa, kazi iliyofanyika kwa miaka miwili na nusu tangu mradi kuanza baada ya mabadiliko imefanyika kwa mwaka mmoja," alisema.

Katika ziara yake kwenye mradi huo jana, Waziri Makamba alifuatana na wajumbe wa Bodi ya TANESCO, watendaji wa shirika hilo na waandishi wa habari walitembelea maeneo muhimu kwa mradi huo.

Mhandisi Mkazi Mwandambo alisema utekelezaji wa mradi huo unaenda sambamba na ujenzi wa daraja la kisasa litakalounganisha Mkoa wa Pwani na mikoa ya Kusini ambalo limefikia asilimia 96.

Mradi huo ulioibua mijadala mingi kitaifa na kimataifa kutokana na hisia za kutokea madhara ya kimazingira, ulianza kutekelezwa Desemba 2018.

Rais wa wakati huo, Hayati Dk. John Magufuli, aliitoa hofu Jumuiya ya Kimataifa kwamba mradi huo unakwenda kuyanusuru mazingira kwa kuwa utazalisha umeme mwingi utakaopunguza matumizi ya kuni na mkaa nchini.

Mradi huo ni mkubwa zaidi katika uzalishaji wa umeme Afrika Mashariki na unashika nafasi ya nne barani Afrika kwa uzalishaji wa umeme. Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, Maharahe Chande, akijibu maswali ya waandishi wa habari waliohoji kuhusu madhara ya mradi huo kimazingira, alisema ni hatari zaidi kutotekeleza mradi huo kuliko kuutekeleza.

Alisema ni muhimu kiuchumi katika kuwezesha ujenzi wa viwanda, bali pia kwa mazingira kutokana na jamii kukata miti ili kupata nishati.

Chande alibainisha kuwa mradi huo kwa sasa umetoa ajira 11,060 na waajiriwa wa mradi huo asilimia 90 ni Watanzania.

Aprili 10, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, alipotembelea mradi huo alisema serikali itaendelea kutoa fedha za kugharamia ujenzi huo unaotarajiwa kukamilika Juni 2024.

## Bil. 39/- kukarabati vyuo 4 vya ualimu

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

ZAIDI ya Sh. bilioni 39.7 zimetumika kuboresha miundombinu ya vyuo vya ualimu vinne nchini ili kuviwezesha kuandaa walimu watakaokwenda kuandaa Watanzania wenye ujuzi na kuingia kwenye soko la ajira.

Akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Rungwe, wakati wa ziara ya kutembelea miundombinu iliyojengwa na kukarabatiwa ya vyuo vinne, Rais Samia Suluhu alisema lengo la kazi hiyo ni kuondoa kero zinazotolewa na wananchi kuhusu elimu kwa vijana.

Rais Samia alisema wananchi wanalalamika kuwa elimu inayotolewa haitoi ujuzi unaowawezesha kushindana kwenye soko la ajira.

"Wananchi mmekuwa mkilalamika kwamba tunawachukua vijana wenu na kukaa nao kwa miaka mingi na tunawarudisha na karatasi ambayo haiwapi uwezo wa kuajiriwa ama kujiajiri kwa kuwa hawana ujuzi walioupata kwa miaka yote, hivyo maboresho haya yanalenga kutatua changamoto hii," alisema Rais Samia.

Alisema kuwa ujenzi na ukarabati wa miundombinu hiyo unakwenda sambamba na maboresho ya mitaala na mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2914 yanayotupeleka katika elimu ujuzi.

Aliishukuru Serikali ya Canada kwa ufadhili wa mradi uliotumika kujenga na kukarabati miundombinu hiyo, huku akiipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa usimamizi mzuri wa mradi huo.

Awali, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema mradi umetekelezwa kwa ushirikiano wa serikali na Canada ambayo ilitoa Sh. 30,952,925,648.41 na Tanzania Sh. 8,846,876,095.43.

Alisema ukarabati umehusisha Chuo cha Ualimu Mpuguso, Mbeya, Chuo cha Ualimu Kitangali, Mtwara, Chuo cha Ualimu Ndala, Tabora na Chuo cha Ualimu Shinyanga, kwa kujenga mabweni, madarasa, mabwalo, maktaba, maabara na mifumo ya majisafi.

Naye Balozi wa Canada nchini, Balozi Hellen Fytche, alisema Serikali ya Canada itaendelea kushirikiana na Tanzania kuboresha upatikanaji wa elimu bora ya elimu ya msingi, sekondari pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu katika vyuo vya ualimu kwa ajili ya kuwanoa walimu.

Alisema Canada inaamini maboresho hayo yatasaidia kufikia lengo namba nne la Malengo Endelevu ya Milenia (SDG), linalohakikisha elimu jumuishi na linganifu inayotoa fursa za kujifunza kwa usawa kwa wote.

Serikali inamiliki vyuo vya ualimu 35 vilivyojengwa miaka mingi iliyopita kiasi cha miundombinu yake kuwa chakavu na ndiyo maana serikali imeamua kukarabati.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na mkewe Mama Mariam Mwinyi (katikati), wakipata maelezo yaliyotolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uratibu wa Uchumi wa Buluu, Hamad Bakari Hamad (wa tatu kulia), wakati walipotembelea maonesho ya wakulima Nanenane viwanja vya Kizimbani Wilaya ya Magharibi "A" Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja jana. Wengine ni Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis (kushoto), Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said. **PICHA: IKULU**

## Simbachawene ataka Uwanja wa Nanenane uboreshwe kimataifa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Uratibu na Bunge, George Simbachawene, amezitaka sekta za Uvuvi, Mifugo na Kilimo kuboresha Uwanja wa Maonesho Nanenane Kanda ya Mashariki na kutumika kimataifa.

Simbachawene alitoa agizo hilo jana wakati akifunga maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere na kuwa uwanja huo umetumika kwa muda mrefu na kuwa na uwezo wa kuonesha kimataifa kutokana na elimu na teknolojia zinazotumika kutoa elimu.

Alitoa rai kwa wizara husika kuchukua hatua stahiki kuimarisha uwanja huo ikiwamo ujenzi wa uzio na kuboresha baadhi ya miundombinu inayohitaji matengenezo madogo madogo.

Aliwahamasisha wakulima mkoani hapo umuhimu wa kulima zao la kahawa kutokana na kuonekana linakubali mkoani Morogoro baada ya banda la maonesho la Tanga kupanda na kustawi kwa kasi.

Alisema ni wakati umefika kwa wakulima wa mkoa huo kulima kahawa ambayo ina soko zuri na inakubalika dunia nzima na kuanza kuwauzia wateja wao hasa maeneo ya Msamvu stendi ambako wao huwauzia kwa wingi wa ndizi.

Aidha, aliagiza shughuli zinazofanyika kwenye uwanja huo ziwe endelevu na kufikisha kwa walengwa teknolojia na ubunifu ulioko kwenye uwanja huo.

Simbachawene aliwakumbusha wananchi kushiriki Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu kwa ajili ya kupanga shughuli za maendeleo ikiwamo ya kilimo na mifugo.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatuma Mwasa, alisema serikali imedhamiria kutenganisha maeneo ya wakulima na wafugaji ili kuondoa migogoro kati ya sekta hizo muhimu katika kuongeza uzalishaji na kukuza uchumi wa taifa.

Akitoa salamu za mkoa huo, Mwasa alisema lengo la maonesho ya Nanenane ni jamii kujifunza na kupata elimu zitakazosaidia kufanya shughuli za ufugaji, kilimo na uvuvi na kuleta tija katika uzalishaji wa bidhaa bora.

Maonesho hayo yamehudhuriwa na halmashauri zipatazo 34 na washindi watatu wa jumla wa maonesho hayo ni Bodi ya Pamba iliyoshika nafasi ya kwanza, ya pili ni Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na ya tatu ni Farmbase Tanzania Ltd.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sikukuu ya Wakulima ilete suluhisho sekta ya kilimo

**JANA** ilikuwa maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima inayofahamika kwa jina maarufu la Nanenane ambayo husherehekewa nchini kote kila mwaka Agosti 8.

Sherehe hiyo, inatayarishwa na kuratibiwa na Wizara ya Kilimo na kuhusisha taasisi, wizara na mtu mmoja mmoja katika sekta ya kilimo.

Maadhimisho hayo yalifanyika katika mikoa na kanda mbalimbali ambako wakulima walionyesha kazi zao kwa waliotembelea maonyesho hayo.

Huu ni mwendelezo wa maadhimisho ya kila mwaka, wa wizara na taasisi zake kuonyesha kazi za kilimo, namna gani wanafanya kazi za kuboresha sekta hiyo nchini.

Ndiyo maana pamoja na mambo mengine kunakuwa na mashamba darasa, kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma.

Unapotembelea maonyesho hayo utapata tumaini kwamba, kuna uwezekano kabisa wa kuwa na kilimo chenye tija kwa wakulima, kutokana na mashamba, mfano kuandaliwa kwa ustadi mkubwa na yamestawi vyema.

Historia ya sherehe hizo zilianzishwa na Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, alipokuwa madarakani mwaka 1993, lengo kuu likiwa ni kuonyesha mazao, mifugo inayozalishwa na wakulima hapa nchini.

Pia sherehe hizo kwa desturi iliyowekwa na serikali huadhimishwa kila mwaka kwa kuzunguka katika mikoa, kwa mwaka huu maadhimisho hayo yamefanyika mkoani Mbeya na yalifunguliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na kufungwa jana na Rais Samia Suluhu Hassan.

Katika maadhimisho hayo kampuni na taasisi mbalimbali za serikali na binafsi zimejitokeza kwa wingi kushiriki, huku baadhi yao zikiwa na mashamba darasa ya kuonyesha mazao na mifugo.

Baadhi ya taasisi kama ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), ilionyesha mkungu wa ndizi aina ya Fhia (ndizi Bukoba) yenye kilo zaidi ya 100 ambayo ilikuwa kivutio kikubwa kwa wakulima na wananchi waliojitokeza katika maadhimisho hayo.

Hakika sherehe hizo kwa mwaka huu zilifana na zilitoa somo kwa washiriki walioweza kufika katika mabanda yao kwa kupata elimu ya kilimo, ufugaji na hata ya kibiashara.

Licha ya jitihada za serikali za kuwainua wakulima tunaamini kwamba masoko ya mazao ni suala muhimu katika jitihada za kuchochea kilimo nchini ili kitoe mchango unaostahili katika uchumi nchini.

Kuwapo kwa masoko ya uhakika kwa ajili ya mazao kunawatia moyo na kuwachochea wakulima kulima na kuzalisha mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula na biashara. Pale inapotokea pakakosekana masoko, hali hiyo huwaathiri wakulima kwa namna mbalimbali.

Mosi, wanalazimika kuuza mazao yao kwa bei ndogo na pili, hawauzi kabisa, hivyo kubaki nayo.

Katika hali kama hii wakulima wanapata hasara kwa kuwa wanakuwa wametoa gharama kubwa za pembejeo pamoja na muda. Matokeo yake ni kukata tamaa na kuamua kuachana na kilimo cha zao husika.


Kwa mfano, kulikuwapo na malalamiko kutoka kwa wakulima wa mahindi mkoani Rukwa miaka ya nyuma kuwa wanakabiliwa na matatizo ya kukosa soko la uhakika la kuuza mahindi yao.

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inapaswa kutatua matatizo sugu yanayolalamikiwa na wakulima kila mwaka ikiwamo kutopelekwa kwa wakati pembejeo za kilimo hata kujikuta wakishindwa kuzalisha mazao mengi, hivyo kujikuta wakipata hasara kinyume na matarajio yao.

Licha ya kushindwa kupata pembejeo kwa wakati, matatizo mengine wanayolia ni kushindwa kupata mbolea kulingana na mahitaji yao.

Ni matarajio yetu kuwa wahusika kwa maana ya Wizara ya Kilimo ambayo ni sikivu na wachapakazi, watayafanyia kazi matatizo hayo ili siku moja wakulima nao wacheke, lengo likiwa ni kuongeza hamasa ya uzalishaji zaidi katika sekta ya kilimo nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Pankras Luoga

# Lala salama sensa, wataalamu watumike kuelezea faida

**TANZANIA** itafanya sensa ya watu na makazi mwezi huu Jumanne Agosti 23, watu wote wa Bara na Zanzibar wakitarajia kuhesabiwa.

Ni sensa ya sita kufanyika huku ikitanguliwa na zile za miaka ya 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012. Wakati ni kipindi cha lala salama, uhamasishaji wa sensa unaelekea kukamilika.

Ili kufanikisha, serikali ilianza maandalizi kwa kuunda tume ya sensa yenye jukumu la kuratibu shughuli zote inayoongozwa na Mwenyekiti Anne Makinda, Spika mstaafu.

Mpaka sasa tume imefanyakazi mbalimbali za uratibu ikiwa ni pamoja na kuendesha sensa ya majaribio na kufundisha makarani watakaoendesha zoezi hilo nchini.

Hivyo, kwa hali hii ni sahihi kusema kuwa maandalizi ya sensa hiyo yamekamilika na kinachosubiriwa ni kufika siku hiyo na wananchi washiriki zoezi hilo kikamilifu.

Pia kumekuwa na ujumbe wa kuhimiza ushiriki katika maeneo mbalimbali hasa katika hafla zinazohusisha viongozi wa kitaifa.

Na tumeshuhudia viongozi wetu wa kitaifa wakieleza umuhimu wa kila mwananchi kushiriki zoezi hili muhimu la kitaifa na kutoa taarifa kamili na za ukweli.

Lakini, bado kumekuwa na ukimya kidogo wa wataalamu kutoka sekta mbalimbali kujitokeza kwa jamii na kuelezea na kuichambua sensa kwa mapana yake hasa kuhusu faida katika kuwezesha sekta hizo kutoa huduma bora kwa jamii.

Tunawashukuru viongozi wa dini kwani wameanza na wanaendelea kuwahimiza waumini wao kushiriki zoezi la sena na kuonyesha kuwa siyo kitu kibaya kwani hata vitabu vya dini vimeruhusu.

Nini kifanyike? Wataalamu wa kila sekta nchini wajitokeze na kuieleza jamii faida za kila sensa kwa sekta mhusika katika kuandaa sera na kupanga mipango ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuihudumia jamii.

Wataalamu wa sekta kama afya, elimu, maji, nishati, miundombinu, kilimo, utalii, mifugo na nyingine waende kwa jamii na kueleza faida za sensa.

Wataalamu wawaeleze wananchi kuwa mipango yote hupangwa kwa kutumia takwimu za sensa na pia utoaji huduma huendana na takwimu zinazotokana na zoezi hilo la sensa.

Na zaidi ni kuwa sensa hutoa takwimu zenye kusaidia katika kupata uwiano wa mgawanyo wa rasilimali kwa ngazi au eneo husika nchini. Na kuwa upatikanaji wa takwimu sahihi za sensa utasaidia kufanya tathimini na kufuatilia wa huduma zitolewazo kwa jamii hasa kwa kulinganisha idadi ya wananchi wanaofikiwa na huduma dhidi ya jumla ya wananchi wa eneo husika kutoa huduma inayoakisi matakwa ya watu.

Pia, tathimini ya wataalamu hawa inaweza kuanza sasa ili kujua kama kuna uhitaji wa elimu zaidi ya sensa kwa wananchi au hamasa imetosha na hivyo wananchi wapo tayari kuhesabiwa .

Nini faida za wataalamu wa kila sekta kuhamasisha ushiriki wa sensa? Kuna faida nyingi za kuwatumia wataalamu hawa kutoka sekta mbalimbali kwenda kuhamasisha wananchi kushiriki. Mojawapo ni kuwa wataalamu hawa wapo karibu na wanaishi na jamii na hivyo kuijua vizuri. Na kutokana na wataalamu hawa kuwa karibu na jamii hivyo wananchi wanawaamini.

Basi kuwatumia hawa walioaminiwa tayari na jamii ni njia rahisi zaidi katika kuwafikia wananchi na kuhakikisha wanapokea ujumbe na hivyo kushiriki katika zoezi la sensa itakapofika Jumanne Agosti 23.

Pia itasaidia wananchi kuelewa vizuri faida za sensa kwa kila sekta tena kwa lugha za kawaida zinazoendana na mazingira yao.Pia tathmini ya wataalamu hawa inaweza kuwa na faida katika muda huu wa maandalizi kwa kutoa taarifa za maendeleo ya zoezi la uhamasishaji, kujua kama kuna uhitaji wa elimu zaidi ya sensa kwa wananchi au la. Na kama kweli elimu imetosha na hivyo wananchi wapo tayari kwa kushiriki zoezi hilo itakapo siku iliyopangwa.

Wito wangu ni kuwa, kwa sasa wataalamu kutoka sekta mbalimbali waende kwa wananchi kuwaeleza faida ya kushiriki na kutoa taarifa za ukweli bila kuficha chochote.

Faida hizi zielezwe kwa undani hasa katika sekta husika kwa mfano, wataalamu wa sekta ya afya waende kwa wananchi na kueleza jinsi wanavyoweza kuboresha huduma za afya kama kupanga bajeti halisia za afya kulingana na idadi ya watu katika eneo husika, ujenzi wa vituo vya afya na upangaji wa watumishi wa afya kuendana na takwimu za sensa. Na pia waambiwe hasara za wananchi kutoa taarifa zisizo za ukweli au kutoshiriki kabisa kwenye zoezi hilo la sensa.

Mwandishi ni mhadhiri Msaidizi (Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya Miradi ya Afya) Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili.
**Mawasialino :0757645746.**

# Kundi maalumu latakiwa kuchangamkia asilimia 30

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MAMLAKA ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), imewahamasisha wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu kuchangamkia fursa ya asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi ya serikali inayotengwa kwa ajili yao kama makundi maalum.

Hamasa hiyo ilitolewa na Ofisa Uhusiano kwa Umma Mkuu wa PPRA, Zawadi Msalla, alipozungumza na waandishi wa habari katika banda la mamlaka hiyo kwenye maonesho ya wakulima maarufu Nanenane yanayofanyika kitaifa jijini Mbeya.

Zawadi alisema kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura namba 410, taasisi zote zinapaswa kutenga asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi ya mwaka kwa ajili ya makundi maalum.

Alisema kiwango hicho kinachotengwa na serikali ni fursa kubwa inayoweza kuwainua kiuchumi ikiwa ndiyo dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Hii ni fursa adhimu inayotolewa na serikali na ikitumika ipasavyo tutaongeza wigo wa ajira. Ukichukulia mfano wa mwaka wa fedha uliopita, jumla ya bajeti ya ununuzi ya serikali ilikuwa takribani Sh. trilioni 22, ambayo asilimia 30 ni takribani Sh. trilioni 6.6," alisema na kuongeza:

"Zabuni za thamani hii zote zilitengwa kwa ajili ya makundi maalum kwa mwaka huu tunaamini itaongezeka."

**Alisema kiwango hicho kinachotengwa na serikali ni fursa kubwa inayoweza kuwainua kiuchumi ikiwa ndiyo dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan.**

# Waziri Ulega aonya migogoro, mitafaruku vyama vya ushirika

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI imewataka viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika nchini, kutenda haki wanapotekeleza majukumu waliyokabidhiwa na wanachama kwa uadilifu ili kujenga imani kwao na serikali iliyopo madarakani.

Rai hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alipokuwa akizungumza kwa nyakati tofauti na watumishi wa vyama vya ushirika, alipotembelea maonesho ya wakulima (Nanenane), Kanda ya Kusini, Manispaa ya Lindi.

Vyama alivyovitembelea ni pamoja na Lindi Mwambao na RUNALI vya mkoani Lindi, TANECU na MAMCU vya Mtwara.

Akizungumza na watumishi wa vyama hivyo, Ulega alisema migogoro na mitafaruku inayotokea kwenye ushirika, huchangiwa na usiri unaofanywa na baadhi ya viongozi na watendaji wao wa kutoshirikisha wanachama katika mambo mbalimbali, zikiwamo kuficha taarifa zinazotakiwa wazitambue.

Naibu Waziri Ulega alisema njia pekee ya kuepusha migogoro na mitafaruku ni pamoja na viongozi kutekeleza majukumu waliyopewa kwa uadilifu, hali itakayowasaidia wanachama na wakulima kuwajengea imani na serikali iliyoko madarakani.

"Jamani ushirika unapata tabu sana, tatizo ambalo husumbua hadi serikali," alisema Ulega.

Vile vile, alisema wakulima wanapokosa imani na vyama vyao vya ushirika kwa kuhisi wanaibiwa mazao yao, hali hiyo haishii kwa viongozi pekee bali hukichukia chama kilichoko madarakani pia.

Alisema viongozi na watendaji wanapofanya kazi vizuri wanaisaidia serikali kuepusha migogoro na mitafaruku ndani ya ushirika na jamii wakiwamo wakulima.

Pia aliwasisitiza wakuu wa wilaya wote nchini kuwatumia sheria wanaotekeleza majukumu yao, ikiwamo kuwachukulia hatua za kuwafikisha kwenye vyombo vya dola wale wanaobainika kwenda kinyume na taratibu za ushirika.

Akipokea agizo hilo kwa niaba ya vyama hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, Halima Chaurembo, amemhakikisha Naibu Waziri Ulega kuwa wanaisimamia na kuilinda sheria, ikiwamo kuwafikisha mahakamani wote watakaokwenda kinyume na taratibu zilizowekwa.



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma akisalimiana na wafanyakazi wa mfuko huo walioshiriki kutoa huduma kwa wanachama na wananchi wakati wa maonyesho ya Nanenane kwenye viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kahama kunufaika mradi WB barabara za kisasa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MRADI wa Uboreshaji Miundombinu katika miji nchini (TACTIC), unatarajia utekelezaji katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama Septemba, mwaka huu kwa kujenga barabara yenye urefu wa kilometa saba maeneo ya mjini na kilometa 12.6 eneo la Viwanda Zongomela.

Mradi huo ulizinduliwa mwaka jana katika kikao kilichohusu mpango wa uboreshaji wa miundombinu katika miji nchini kupitia mpango wa Benki ya Dunia na Manispaa ya Kahama ni moja ya eneo la utekelezaji kwa kila barabara kuwa na taa.

Benki ya Dunia imetenga Dola za Kimarekani milioni 500 (Sh. trilioni 1.5) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambao utahusisha ujenzi wa barabara, mitaro na vituo vya mabasi huku Kahama ikitarajiwa kujenga barabara za urefu wa kilometa saba maeneo ya mjini, kilometa 12.6 eneo la Viwanda Zongomela.

Katika utekelezaji wa mradi huo wananchi walitakiwa kuwa makini ili kuepukana na maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi na kutoanzisha migogoro itakayokwamisha utekelezaji wa mradi huo.

Mbunge wa Jimbo la Kahama, Jumanne Kishimba, alibainisha hayo jana katika kikao cha Baraza la Madiwani cha Manispaa ya Kahama cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2021/2022 kilichojadili masuala mbalimbali ya kimaendeleo ikiwamo afya, maji, elimu na miundombinu ya barabara.

Alisema, mradi utaondoa malalamiko kwa wananchi kuhusu ukosefu wa barabara zenye uhakika na hautavunja nyumba yoyote ya mkazi ili kupisha ujenzi wake na kuwataka madiwani kuwaeleza wananchi faida za mradi na kuchangamkia fursa za ajira za muda zitakazotolewa.

Alisema, Kata ya Maengo eneo la sokoni kumekuwa na sintofahamu ya wakazi wa eneo hilo kutaka fidia hali iliyosababisha kutolewa kwenye mradi awamu ya kwanza.

Naye Diwani wa Mhungula, Scolastika Bebete alisema, wanaomba kutumia fedha za mapato ya ndani kwa sasa ili kutengeneza barabara mbovu katika maeneo badala ya kuendelea kutegemea fedha kutoka Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) ambazo zimekuwa zikija chache.

Alisema, wasipotengeneza barabara hizo mwaka 2025 kwenye uchaguzi mkuu wataulizwa na wapiga kura, kama halmashauri inaweza kutenga fedha na kujenga maghorofa kwanini ishindwe kutenga fedha na kurekebisha baadhi ya barabara hizo.

Diwani Iyenye Lucas Makurumo, alishauri halmashauri kununua mitambo ya ujenzi wa barabara kama walivyofanya halmashauri za Msalala na Ushetu kama suala ya mafuta kata zote zitachangia gharama na Kahama inasifa nyingi nje, lakini barabara zake mbovu.

# Shaka ataka mipango kusaidia vijana kifedha

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa** MOROGORO

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, ametoa wito kwa serikali kuweka mipango mizuri kwenye taasisi za kifedha ili kuwasaidia vijana hasa wanaomaliza vyuo vya kilimo.

Alitoa wito huo jana mkoani Morogoro wakati alipotembelea mabanda ya maonesho ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Mashariki, na kwamba taasisi za fedha alizozitembelea zimeonyesha nia ya kusaidia vijana.

"Wito kwa Wizara ya Kilimo na serikali fedha zinazotengwa na mashirika ya fedha kuweka mpango mzuri kwaajili ya kuwasaidia vijana hao hapa Morogoro kuna chuo cha kilimo tukiwekeza itasaidia hawa vijana na kuwatambua maeneo wanayotoka na serikali kuweka maeneo maalumu mfano akipatiwa hekta na taasisi za fedha zikitoa fedha zinamsaidia," alisema.

Shaka alisema, anaamini wakifanya hivyo itasaidia kutatua changamoto ya ajira kwa kiasi kikubwa na hilo linawezekana wajifunze kwa nchi ya Misri ambayo imeweza na Tanzania inaweza zaidi.

"Lazima kuwapo na mipango madhubuti ya kuhakikisha kuwa vijana hao wanawaandaa hadi wanapoingia katika soko la ajira wamejitahidi kuonyesha uwezo wao katika kuwekeza sekta ya kilimo," alisema Shaka.

Aidha, alisema maandalizi ya maonyesho hayo ameshuhudia kuwapo na uboreshaji mkubwa na hayo yamechochewa na utayari wa viongozi katika kutafsiri kwa vitendo dhana na dhamira waliyonayo ya kusimamia maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema, kilimo ni uti wa mgongo kwa taifa na wanakitegemea kwa asilimia 70 ndani ya nchi katika kuendesha maisha na kwa uchumi wa nchi.

Shaka alisema, Rais Samia anatazama sekta ya kilimo kama mkombozi kwa Watanzania na amepanga kufanya mapinduzi makubwa na ndiyo maana wameongeza fedha katika bajeti ya mwaka 2022/23 ikilinganishwa na mwaka jana.

"Ilani ya chama iliahidi katika kipindi cha miaka mitano watazalisha ajira milioni nane kwa Watanzania tayari wamejiwekea matarajio ifikapo mwaka 2025 sekta hii itazalisha zaidi ya ajira milioni tatu haya ni mageuzi makubwa," alisema Shaka.

Aidha, Shaka aliwashauri wakulima wakati umefika wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi, hiyo itasaidia kuona ni namna gani ya kukabiliana na jambo hilo ili kukuza sekta hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya Kaimu wa Mkoa wa Morogoro ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Jabiri Makame, alisema maelekezo waliyopewa wataenda kuyafanyia kazi ili kuboresha shughuli za kilimo



Baadhi ya wanafunzi walipotembelea shamba la maonesho ikiwa sehemu ya kujifunza kupitia mradi wa viungo katika maonesho ya Nanenane Kizimbani Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Vyuo 60 vya VETA kujengwa nchini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 168.7 mwaka wa fedha wa 2021/2022 na 2022/2023 kwa ajili ya kujenga vyuo 60 vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), wilaya mbalimbali nchini.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Anthony Kasole, alisema hayo jana, wakati Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokagua na kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Ikungi alipokagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika mkoa huo.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 imeshatoa Sh. bilioni 68.7 kwa Wizara ya Elimu kwa ajili ya ujenzi wa vyuo 25 vya VETA vya wilaya nchini mojawapo ikiwa ni Wilaya ya Ikungi.

Kasole alisema ujenzi wa Chuo cha VETA Ikungi, serikali imetoa Sh. bilioni 2.3 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na pia serikali imeongeza Sh. milioni 893 za UVIKO-19, kwenye ujenzi wa chuo hicho.

"Mradi wa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Ikungi kutajengwa majengo 17 na tumepata eneo lenye ukubwa wa ekari 50 ambapo hati imeshatolewa," alisema.

Kasole aliongeza kuwa katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 serikali imetoa Sh. bilioni 100 ambazo zitatumika kujenga vyuo vingine 35 katika wilaya pamoja na chuo kimoja chenye hadhi ya mkoa ambacho kitajengwa katika Mkoa wa Songwe.

Alisema Chuo cha VETA Ikungi kitakapokamilika Septemba mwaka huu, kitaanza kutoa mafunzo ya kozi ya muda mfupi kwa wanafunzi kuanzia Oktoba hadi Januari udahili wa wanafunzi wa kozi ndefu utakapofanyika.

Aliongeza kuwa chuo hicho kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 240 watakaokuwa wanasoma masomo ya muda mrefu na kati ya hao 144 watakuwa bwenini na 96 wa kutwa.

Aidha, alisema serikali imetoa Shilingi bilioni nane kwa ajili ya kutengeneza samani za ofisini, mabweni na madarasani kwa ajili ya vyuo 25 na kazi ya kuzitengeneza samani hizo inafanywa na chuo cha kutengeneza samani kilichoko Dodoma na kwenye karakana za vyuo vingine vilivyoko nchini.

Alisema katika mradi jumla ya samani 39,000 zitatengenezwa zilizokwishatengenezwa zimeanza kupelekwa katika baadhi ya vyuo ambavyo ujenzi umeshakamilika.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa elimu ya ufundi na hivyo kutuongezea bajeti ya ujenzi wa vyuo vya VETA ambavyo vitakuwa mkombozi mkubwa kwa vijana kuweza kusoma na kujiajiri," alisema.

Naye Waziri Mkuu, Majaliwa aliagiza ujenzi wa chuo hicho ukamilike kwa wakati kulingana na mkataba ili masomo yaweze kuanza haraka katika chuo hicho.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro, aliimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuijali na kuithamini wilaya hiyo kutokana na kutoa mabilioni ya fedha ambayo yamewezesha utekelezaji wa miradi katika sekta ya elimu, afya, maji na barabara.

## Mtoto afariki dunia madai ya kunyweshwa sumu na mwenzake

**Na Said Hamdani,** LINDI

MTOTO Suleiman Hamisi, mwenye umri wa miaka mitatu na miezi minane, Kijiji cha Mnyangara, Wilaya ya Lindi, amefariki dunia na mwingine Mohamedi Zuberi (3) amehamishiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa madai ya kunyweshwa sumu na mtoto mwenzao mwenye umri wa miaka minne (jina limehifadhiwa).

Suleiman alifariki katika Hospitali ya Sokoine mkoani Lindi, alikokuwa akipatiwa matibabu Julai 20, mwaka huu, baada ya kudaiwa kunyweshwa sumu inayoelezwa kutumika kuua wadudu wanaoshambulia zao la korosho.

Taarifa kutoka kijijini hapo na kuthibitishwa na baba wa watoto hao, Hamisi Selemani na Zuberi Namtendele, zinasema mtoto huyo anadaiwa kuwanywesha sumu hiyo watoto wenzake baada ya kwenda kuichukua nyumbani kwao.

Wazazi hao walidai mtoto huyo mwenye sifa ya utundu, aliwanywesha wenzake sumu hiyo walipokuwa wanacheza pamoja asubuhi.

"Hawa watoto walikuwa wanacheza ndipo mwenzao akaenda ndani ya nyumba yao na kuchukua sumu na kuwanywesha wenzake," alidai mmoja wa wazazi.

Pia walidai baada ya kuwanywesha sumu hiyo, alichukua kiwembe na kuanza kuwanyoa nywele wenzake ambao aliwasababishia majeraha kutokana na kuwakatakata.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Sokoine, Dk. Mohamedi Muhaji, alipotafutwa kupitia simu yake ya mkononi ili kupata taarifa za watoto hao, iliita bila ya kupokewa, lakini mmoja wa wauguzi ambaye hakupenda jina lake litajwe gazetini kwa kuwa sio msemaji, alikiri kupokea watoto hao.

Alisema, Suleiman alifariki Julai 20, alipokuwa akipatiwa matibabu, wakati Mohamed amepoteza sauti kutokana na koo lake kushambuliwa na sumu hiyo na kulazimika kuhamishiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa matibabu zaidi.

Muuguzi huyo alisema, Mohamed alilazwa chumba cha uangalizi maalumu (ICU), Hospitali ya Sokoine na kupewa uhamisho Julai 24, kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

"Huyu mtoto Mohamed amekosa sauti kwani alikuwa anakoroma tu, sauti haitoki hivyo amelazimika kuhamishiwa Hospitali ya Muhimbili," alisema muuguzi huyo.

# Waajiri viwandani wakumbushwa kuthamini, kujali wafanyakazi

Na Frank Monyo

SERIKALI imewataka wamiliki wa viwanda nchini kujali na kuilinda nguvukazi inayotumika ili kuwa na uzalishaji endelevu na wenye tija kwa maendeleo endelevu ya taifa.

Tamko hilo limetolewa jana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, alipofanya ziara katika viwanda mbalimbali mkoani Dar es Salaam, akiwa ameambatana na maofisa wa Taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwamo Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA). Katambi alisema malengo ya serikali ni kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia uzalishaji viwandani na kwamba serikali inawajibika kujenga mazingira bora ya biashara na uwekezaji.

"Serikali inajitahidi kuhakikisha kunakuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji pamoja na kuhakikisha kwamba shughuli zote za uwekezaji zinazingatia sheria za nchi ikiwamo Sheria za Ajira na Mahusiano Kazini, Usalama na Afya Mahali pa Kazi na hifadhi kwa jamii," alisema Katambi na kuongeza:

"Katika ziara hii ya leo (jana) tumefanya ukaguzi wa kushtukiza katika viwanda vitano vinavyozalisha bidhaa mbalimbali zikiwamo za plastiki, tumebaini upungufu katika viwanda husika, ikiwamo mazingira ya kazi yasiyo rafiki kwa wafanyakazi na uwapo vitendo vya unyanyasaji kwa wafanyakazi."

Alitoa rai kwa waajiri nchini kutoa ajira zenye staha ili kuendana na sheria za nchi pamoja na mikataba ya kimataifa ambayo nchi imeridhia.

Kaimu Meneja wa Kanda ya Pwani wa OSHA, George Chali, aliainisha changamoto za usalama na afya zilizobainika katika ziara hiyo zikiwamo ukosefu wa vifaa kinga miongoni mwa wafanyakazi, uwapo wa nafasi finyu za kufanyia kazi, wafanyakazi kutekeleza majukumu yao katika mtindo usiofaa kiusalama na afya (ergonomic issues).




Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akizungumza wakati wa mkutano na waandishi wa habari kuhusu ushiriki wa Benki ya NMB kwenye maonyesho ya Nanenane jijini Mbeya. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Kilimo Biashara wa NMB, Isaac Masusu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TALIRI yakamilisha utafiti kuboresha ufugaji asilia

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema ipo katika hatua za utafiti wa mifugo utakaowezesha wafugaji kufuga kwa kutumia virutubisho asilia.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Prof. Erick Komba, wakati wa maonesho ya wakulima (Nanenane) yanayofanyika kitaifa jijini Mbeya, akiwa katika banda la Wizara ya Mifugo.

Komba alisema TALIRI kwa sasa inashirikiana na Kampuni ya Afrint Bio Solution ya nchini Indonesia, inayotengeneza bidhaa zisizotumia kemikali yoyote bali virutubisho asilia visivyohitaji mnyama kutumia dawa wala chanjo yoyote tangu kuzaliwa hadi kukua kwake.

Alisema serikali inaelekea kupata ufumbuzi wa magonjwa mbalimbali ya mifugo kwa kutumia virutubisho asilia visivyo na kemikali vinavyosaidia ukuzaji mnyama kwa haraka na kukuza uchumi wao.

Kwa upande wake Rais wa Kanda ya Afrika wa Kampuni ya Afrint Bio Solution, Paluku Emmanuel, alisema wamekuwa wakifanya majaribio ya kufuga kuku bila kutumia chanjo yoyote na kwamba kuku hao wamefikia uzito wa kilogramu mbili kipindi cha mwezi mmoja na nyama yake haina mafuta mengi.

Alisema virutubisho hivyo asilia pia vimekuwa vikitoa matokeo mazuri kwa ng'ombe na kuku wa mayai kwa kuongeza uzalishaji wa maziwa na mayai.

"Naomba serikali kushirikiana na kampuni hiyo ili kuongeza tija katika sekta ya mifugo kwa wafugaji kufuga kwa tija na gharama nafuu," alisema.

John Mwakangale, aliyetembelea maonyesho hayo alisema wamefurahia kujionea teknolojia mbalimbali za ufugaji ikiwamo ya kuku na mifugo mingine bila kutumia dawa wala chanjo.

# Serikali yapongeza TARI uzalishaji mbegu bora

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, amesema serikali inatambua jitihada za Watafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kwa mchango wa kuzalisha mbegu bora za teknolojia ya kisasa za kilimo na kuagiza Wizara ya Kilimo kuhakikisha zinawafikia wananchi.

Balozi Kattanga aliyasema hayo jana baada ya kutembelea banda la Wizara ya Kilimo na taasisi zake kwenye maonesho ya wakulima na wafugaji ya Nanenane yaliyofikia kilele jana jijini Mbeya.

Alisema kazi kubwa imefanywa na watafiti wa vituo 17 vya TARI vya kugundua mbegu hizo za teknolojia ya kisasa ambazo zinaongeza uzalishaji na ukindhani na magonjwa kilichobaki sasa ni wakulima kuendelea kuhamasishwa ili wazitumie kwa ajili ya kuleta tija katika sekta ya kilimo.

"Wote tumeshuhudia hapa baada ya kutembelea banda la TARI jinsi utafiti wa mbegu bora na zenye kuongeza tija katika kilimo ulivyofanywa na watafiti wetu wa ndani kilichobaki sasa ni wakulima kuhamasishwa kuzitumia na nyinyi waandishi wa habari tusaidieni kuwaambia," alisema.

Balozi Kattanga alisema ajenda ya serikali kwa sasa ifikapo mwaka 2030 sekta ya kilimo iweze kutoa mchango kwenye Pato la Taifa la asilimia 10 na kwamba mikakati mbalimbali tayari imeshawekwa kufikia lengo hilo.

Awali, akitoa taarifa kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema kwenye kilimo tatizo kuu lililoko ni tija ndogo na kufanya wakulima kulima kilimo cha kujikimu kutokana na kutumia mbegu za kawaida.

Alitoa mfano kwenye kilimo cha zao la mihogo kwa sasa mkulima anapata tani nane za zao hilo kwa hekta kutokana na kutumia mbegu za kawaida, akitumia mbegu zilizofanyiwa utafiti na TARI tija yake itahama na kupata zaidi ya tani 40 kwa hekta na kuongeza uzalishaji mara tano zaidi.

Dk. Mkamilo alisema katika zao la viazi vitamu linalolimwa zaidi na wakulima walioko katika ukanda wa ziwa ambao kwa sasa wanapata tani 4.5 kwa hekta kwa kutumia mbegu zao za kawaida na wakitumia mbegu zilizofanyiwa utafiti tija itahama hadi kufikia tani 10 mpaka 20 kutegemea na mbegu atakazochagua kutumia.

# Mradi kudhibiti sumukuvu kuelimisha wakulima uhifadhi

**Na Renatha Msungu,**
MBEYA

WIZARA ya Kilimo inatekeleza mradi wa kudhibiti sumu kuvu wenye thamani ya Sh. bilioni 80 ambao umelenga kuwaelimisha wananchi kuhifadhi chakula katika hali ya usalama ambayo haitaruhusu sumu kuvu kuingia kwenye mazao.

Mtaalamu kutoka Wizara ya Kilimo, Mercy Buta, alisema hayo katika maonesho ya wakulima Nanenane yanayoendelea kitaifa katika Viwanja vya John Mwakangale, jijini hapo.

Buta alisema, mradi huo unatekelezwa kwenye mikoa 10 na katika halmashauri 18, pia unatekelezwa Zanzibar katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Alisema, lengo la mradi huo ni kuimarisha usalama wa chakula ndani na nje ya nchi pamoja na afya ya jamii.

"Tupo hapa Mbeya kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu sumu kuvu ambayo inayosababishwa na kuvu (fangus)," alisema Buta.

Kuhusu madhara ya sumu kuvu, mtaalamu huyo alisema, madhara yake mtu akila kwa muda mrefu chakula chenye sumu hiyo matokeo yake ni kupata saratani.

"Kansa zinazoripotiwa asilimia 30 inaweza kuwa zinasababishwa na sumu kuvu, ndiyo maana mradi wa kuelimisha jamii umekuja ili kukabiliana na suala hilo," alisisitiza.

Vile vile, alisema katika kudhibiti sumu kuvu, wizara imekuja na teknolojia mbalimbali zinazoweza kudhibiti vikiwamo viuatilifu pamoja na teknolojia nyingine katika kuhifadhi mazao tangu wakati wa kilimo mpaka kuhifadhi mazao. Kwa upande wake, mtaalamu wa kutoka Wizara ya Kilimo, Hilda Shegembe, alisema moja ya teknolojia ni kipukucho mahindi ambayo ni teknolojia rahisi inayoweza kudhibiti sumu kuvu na bei yake ni rahisi.

"Hiki ni kwa ajili ya wakulima wadogo ambao wamekuwa wakipukucha mahindi yao kwa kuyapiga, hii ni hatari kwa usalama wa chakula kwa sababu wakati wa kuyapiga yapo yanayopasuka, hayo yanayopasuka husababisha wadudu wa sumukuvu kuingia katika mazao," alisema Shegembe.

Naye mtaalamu kutoka wizara hiyo, Pendo Nsanya, alisema teknolojia nyingine ni ya kipima unyevu ambayo inatumika kwa kuonekana kwa rangi na humsaidia mkulima kujua kama mazao yake yamekauka ili ayahifadhi badala ya kuhifadhi yakiwa mabichi na kusababisha sumukuvu kuingia katika mazao.

"Kifaa hiki (kadi) kinasaidia kuonyesha mahindi ambayo yamekauka na hivyo kuhifadhi chakula katika hali ya usalama zaidi."



Ofisa Usimamizi wa Fedha, Wizara ya Fedha na Mipango, Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Mary Mihigo, akitoa elimu kuhusu uwekezaji na uwekaji wa akiba kwa wananchi waliotembelea banda la Wizara ya Fedha na Mipango katika maonesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa Uwanja wa John Mwakangale, jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wakulima wahamasishwa kujifunza mnyororo wa thamani

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKULIMA nchini wamehamasishwa kutembelea na kujifunza ujuzi na maarifa kutoka Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) kwa lengo la kukuza na kuboresha mnyororo wa thamani kwenye mazao wanayozalisha.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kaimu Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha, Dk. Cairo Mwaitete, alipozungumza na Nipashe kuhusu mikakati ya kuhakikisha wakulima wanafanya kilimo biashara.

Alisema IAA imeandaa programu maalum ya kuwafundisha wakulima maarifa ya namna ya kuendesha kilimo biashara kwa lengo la kupata faida kupitia masoko na ubunifu.

Alisema hadi sasa tayari programu hiyo inaendeshwa na vijana kutoka maeneo mbalimbali na wamepewa nafasi ya kupeleka mawazo ya kibiashara na wataalamu wa chuo hicho watayaboresha na kuanza kutumika kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.

"Chuo chetu ni cha pekee nchini ambacho kimetoa nafasi kwa vijana kupeleka mawazo yao ya kibiashara na kilimo ambapo jukumu ya chuo ni kuchakata mawazo hayo na kuwasaidia namna ya kufanya katika kuendesha biashara zao," alisema Dk. Mwaitete.

Baadhi ya vijana wanaojihusisha na shughuli za ujasiriamali wamesema kuwa miongoni mwa vikwazo vinavyochangia kushindwa kutimiza malengo yao ni kutokuwa na elimu ya kutosha katika kusimamia na kuendesha biashara zao.

Alisema utaratibu wa Chuo cha Uhasibu Arusha kufungua milango kwa vijana kupeleka mawazo yao ya kibiashara kutasaidia kuboresha na kutoa huduma bora ambazo zitakidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

## Wafugaji washauriwa kujifunza teknolojia bora

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WAFUGAJI nchini wameshauriwa kwenda kujifunza teknolojia bora ya ufugaji na kilimo kwenye banda la Wizara ya Mifugo na Uvuvi, lililoko katika Maonesho ya Wakulima Nanenane Kanda ya Mashariki na kilimo cha majani ya malisho.

Wito huo ulitolewa jana na Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (CCM), Shaka Hamdu Shaka, wakati alipotembelea maonesho hayo kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere nje kidogo ya Manispaa ya Morogoro na kwamba suala la upandaji wa majani ya malisho lina nafasi ya kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji nchini.

Shaka alisema Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kusimamia wizara hiyo pamoja na Wizara ya Kilimo kwa sababu asilimia 85 ya wananchi wanategemea sekta hizo na lazima jitihada zifanywe kuziboresha kwa kuinua kipato cha wananchi.

Aidha, alitoa wito kwa sekta hizo na serikali, kushirikiana na taasisi za kifedha ili kuhakikisha fedha zilizotengwa zinawafikia walengwa na kuwakwamua kiuchumi wakiwamo vijana.

Alisema kutambulika kwa matumizi ya fedha hizo kutaondoa tatizo la ukosefu wa ajira na hadi kufikia mwaka 2023 sekta ya kilimo itakuwa imeajiri wafanyakazi milioni tatu.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Uendelezaji maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo (DGLF), kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi nchini, Rodgers Shengoto, alisema wizara imedhamiria kuinua kipato cha wafugaji kwa kuongeza matumizi ya teknolojia kwenye ufugaji.

Shengoto alisema wizara hiyo kwenye maeneo ya maonesho hayo imeonyesha teknolojia na maarifa mbalimbali kwa wafugaji ikiwamo ya uzalishaji wa mbegu za malisho zinazostahimili hali zote nchini.


Pia, alisema uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki pamoja na zao la mwani na uongezaji thamani kwenye zao la mwani utaongeza tija kwenye uzalishaji wa bidhaa hizo.

Mkulima unapata asali hata wakati wa ukame, iwapo utayazingatia haya



Ukurasa 13

Nipashe
TESA
Jumanne Agosti 9, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

**Kwa watu wanaoishi na ulemavu yajayo yatawafurahisha zaidi**

TEKNOLOJIA
NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA
LINDA MZINGIRA (4)

# Fahamu jinsi 'matangi' haya yanavyotunza maji ardhini

• Tena yanachofanya wakati wa kutengeneza mvua



Ardhi oevu iliyoko msituni ndiyo inayohifadhi maji ardhini na kuwezesha mito kujaa na kutiririsha maji muda wote. **PICHA: MTANDAO**

NANENANE mwaka huu imesheheni kilio uharibifu wa mazingira na ukame ambao ni matokeo ya mabadiliko ya tabianchi. Hakuna kilimo bila maji lakini wakulima, wafugaji na kila mmoja amewahi kujiuliza inawezekanaje mito kutiririsha maji wakati wote?

Ni kwa vipi mwaka hadi miongo kadhaa maji husafiri ndani ya mto? Au mmewaza hivi kuna sehemu yapo matangi ya kuhifadhi maji ardhini? Vipi, mapipa hayo yanafanya kazi gani na yanafananaje?

Makala hii inawapongeza wakulima na wafugaji kwa siku yenu na inawajibu maswali yote hayo. Ukiwa ni mwendelezo wa makala zilizopita kuhusu umuhimu wa misitu na rasilimali nyingine zinazomgusa kila mmoja na kuhimiza ulinzi wa mazingira.

Ukweli ni kwamba, kuna uhusiano wa asili kati ya maji na misitu na hali hiyo ni tangu kuumbwa kwa dunia.

Misitu ndiyo inayotunza na iliyo vyanzo vinavyowezesha mito kutiririsha maji wakati wote na kuchangia ustawi wa maisha ya binadamu kwa kufanikisha kilimo, mifugo, wanyamapori, uvuvi, utalii, usafirishaji na maisha ya viumbe wa majini kama samaki.

Misitu, mvua, na maji ni mihimili mitatu inayounganishwa na nguvu ya asili katika uumbaji, maji ndiyo muhimili mahsusi kwa msingi kwamba maji yanafanya uoto wa asili ikiwamo misitu kuwapo na kuendelea kustawi.

Iwapo sehemu ina uhaba mkubwa wa maji, ardhi inakuwa kame na kavu mno, kiasi cha kuzuia kuota uoto wa asili hapo linakuwa jangwa.

Maji katika bahari, maziwa, mito, mabwawa na ardhi oevu ni chanzo kikuu cha uwapo wa mawingu angani yanayoleta mvua.

Sayansi inaonyesha kuwa kulingana na maumbile ya asili, kuna mzunguko wa maji, yapo majira na nyakati mfano miezi ya ukame (kiangazi) na kipindi cha mvua za masika na vuli, lakini ili mvua inyeshe lazima kuwapo mawingu ya kutosha angani, tena yawe mazito na meusi.

Ikiwa hivyo, ni dalili ya mawingu kusheheni maji mengi na hatimaye mvua kunyesha. Kawaida, jua linapochomoza (mawio) joto huongezeka kadri muda unavyosonga mbele hadi litakapozama (machweo).

Kadhalika, majira ya mvua, joto linakuwa juu na kusababisha unyevunyevu mwingi (high humidity) angani na sehemu za pwani na kusababisha watu kutokwa jasho mara kwa mara.

Ni wakati huo maji baharini, maziwa, mtoni, mabwawa na ardhi oevu kutokana na nguvu ya mionzi ya jua kusababisha joto kuwa juu na kutengeneza mvuke unaojaa hewani, hatimaye kufanya mawingu angani.

**KUHUSU MATANGI**

Tanzania ina maeneo tambarale vilevile ipo milima kama Kilimanjaro, Meru, Livingstone, Rungwe, upo ukanda wa Tao la Mashariki kuanzia Udzungwa hadi milima ya Pare Kaskazini, wilayani Mwanga.

Kuna vilima na milima katika Nyanda za Juu Kusini ikiwamo sehemu ya Mpanga-Kipengere, hususani unapotelemka kuingia Jijini Mbeya utaona vilima na milima mpaka maeneo ya Wilaya za Makete na Ludewa mkoani Njombe hadi Ruvuma.

Vilima na milima ni maeneo yanayokuwa yamefunikwa na misitu minene yenye aina mbalimbali za miti na uoto wa asili wa kutosha.Kitaaluma inajulikana ni misitu-lindimaji (swamp forests) kwa maana kwamba ndiyo 'matangi muhimu ya kuhifadhi maji ya mvua' inaponyesha nyakati za vuli na masika.

Mapipa haya (swamp forests) yapo ndani ya misitu na kila eneo yanapopatikana watu waliyaogopa maana ukiingia huweza kutoka hivyo unazama.Ni ardhi oevu ambayo ilijaa maji miaka yote.

Kimsingi, majira ya mvua yanapowadia na joto kuchochea unyevunyevu kusheheni angani hatimaye upepo uliobeba unyevunyevu kutoka baharini na maeneo mengine yenye maji, huvuma kuelekea nchi kavu na ukifika kwenye miinuko hulazimishwa kupaa juu hadi kileleni.

Huko hukumbana na kizuizi cha misitu minene kiasi kwamba kasi ya upepo hupungua na kusababisha unyevunyevu kutengeneza mawingu mazito na meusi na hatimaye mvua kunyesha kwa wingi.

Uzoefu unaonyesha kuwa milima yenye misitu mikubwa huwa ni vyanzo muhimu vya maji yatokanayo na mvua, chemichemi zinazoanzia misituni hatimaye kuwa mto na mito mikubwa kama Nile (Naili), ambao chanzo chake ni Mto Kagera.

Mfano ni misitu katika Milima ya Uluguru na Udzungwa, mkoani Morogoro, wakati Tanzania inapata Uhuru Disemba 9, 1961 mpaka miaka ya 1970 hadi 1980

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Kwa watu wanaoishi na ulemavu yajayo yatawafurahisha zaidi

• Kufunzwa stadi kujitegemea, kujazwa mikopo

UKOSEFU wa elimu ya ujasiriamali kwa vijana wenye ulemavu, imekuwa tatizo la kujikwamua kiuchumi na kuendesha maisha yao, tena kuishia kuwa tegemezi hata kuitwa omba omba na kubakia watu wa kudharauliwa kwenye jamii.

Ofisi ya Waziri Mkuu, Makazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu, inasema imeuona upungufu huo na imeanzisha programu ya stadi za maisha kwa vijana walio nje ya shule inayotoa elimu ya ujasiriamali kwa makundi maalumu wakiwamo wenye ulemavu.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Vijana Ofisi ya Waziri Julius Tweneshe, anasema lengo ni kuwainua kiuchumi makundi maalumu wanaoshindwa kujingizia kipato kutokana na ukosefu wa elimu ya ujasiriamali na mafunzo ya kujitegemea.

Anaeleza kuwa kutokana kuwapo tatizo hilo, Ofisi ya Waziri Mkuu imeona kuna umuhimu wa kuzunguka maeneo mbalimbali nchini, kukutana na makundi maalumu ya vijana wakiwamo wenye ulemavu na kuwapatia elimu ya ujasiriamali itakayowakwamua kiuchumi.

Wanayofundishwa ni pamoja na usimamizi wa fedha, mbinu za kutambua masoko, matumizi sahihi ya mikopo kabla ya kuvipatia vikundi utaalamu wa kuanzisha miradi yenye tija ambayo itawanyanyua kiuchumi lakini kuwatembelea mara kwa mara na kutoa ushauri.

"Serikali ina fursa nyingi kwa vijana kuwainua kiuchumi, lakini tatizo ni ukosefu wa elimu ya ujasiriamali na kuthubutu, na sisi tumekuja kulitibu hili na tumeanza na vijana, makundi maalumu kutoka hapa Manispaa ya Shinyanga," anasema Tweneshe.

"Mfano, Ofisi ya Waziri Mkuu ina fursa ya mikopo kwa vijana kupitia mfuko wa maendeleo ya vijana ambao kwa sasa umeboreshwa na unatoa mkopo kuanzia kijana mmoja na riba yake imepunguzwa kutoka asilimia 10 hadi tano na vijana wanapaswa kuutumia,"anaongeza.

Anasema, mbali na fursa hiyo ya mikopo kupitia mfuko huo wa mandeleo ya vijana, pia kuna nyingine ya mikopo kwa vijana kupitia halmashauri asilimia 10, ambayo nane hutolewa kwa vijana na wanawake na mbili kwa watu wenye ulemavu.



Kuwawezesha wanaoishi na ulemavu ni kuwapa visaidizi, elimu, stadi za maisha na maeneo ya kufanyia shughuli zao. **PICHA: MTANDAO**

> "Serikali ina fursa nyingi kwa vijana kuwainua kiuchumi, lakini tatizo ni ukosefu wa elimu ya ujasiriamali na kuthubutu, na sisi tumekuja kulitibu hili na tumeanza na vijana, makundi

Masanja Wiliamu, ni kijana mwenye ulemavu ambaye amenufaika na mafunzo hayo ya ujasiriamali, anasema yatakwenda kubadili mfumo wa maisha yake kwa kujishughulisha na ujasiriamali na kuinuka kiuchumi.

Anasema, kwa sasa amepata mwanga wa maisha na kujua wapi pa kuanzia, na kutambua fursa zilizopo kwa vijana ambazo anaweza kuzitumia na kupata mtaji wa kuanzisha biashara zake, na hata kufikia hatua ya kufungua kiwanda kidogo.

"Watu wenye ulemavu tumekuwa tukisahaurika sana katika fursa mbalimbali za kiuchumi, na ndiyo maana ukiangalia wengi hali zetu za maisha ni duni sana, na mara nyingi hua tunategemea kuishi kwa kuomba misaada,"anasema Wiliamu.

"Nimefurahi kupata mafunzo haya ya ujasirimali na nitakwenda kuyatumia vyema kwa kubuni biashara ambayo itanikwamua kimaisha na kuondokana na utegemezi," anaongezea Wiliamu.

Happnes Kasembo, ni mlemavu wa viungo na ni mama wa mtoto mmoja, anasema baada ya kuandamwa na ugumu wa maisha, alianza kufanya biashara ndogo ndogo ili ajikimu kimaisha, lakini imekuwa haikidhi mahitaji yake yote kutokana na ukosefu wa elimu ya kubuni biashara nzuri itakayo mkwamua kimaisha.

Anasema, baada ya kupata mafunzo hayo ya ujasiriamali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, amepata ufumbuzi wa kwenda kubuni biashara nzuri, pamoja na kutumia fursa ya kupata mkopo kupitia halmashauri ili kujiongeza kibiashara na kupata kipato kikubwa.

"Nimekuwa nikifanya biashara ndogo ya kuuza sabuni za vipande, unga, pipi na vitu vingine vidogo vidogo, lakini lengo langu ni kufungua biashara kubwa ili nipate fedha nyingi na kumsomesha mwanangu. Baada ya kupata mafunzo ya ujasiriamali na kuonyeshwa fursa sasa na kwenda kukua kiuchumi,"anasema Kasembo.

Rubeni Simon anasema, kupitia mafunzo hayo malengo yake kwa sasa ni kwenda kununua mashine ya kusaga na kukoboa nafaka, kwa sababu katika maeneo yao ambayo anaishi huko Chibe hakuna mashine hizo, na wananchi wamekuwa wakisafiri umbali mrefu kutafuta huduma hiyo mjini Shinyanga.

"Tunaiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, iendelee kutukumbuka sisi vijana wa makundi maalumu ituwezeshe ili tuondokane na dhana tegemezi sababu uwezo wa kufanya kazi tunao,"anasema Simoni.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Shinyanga John Tesha, anasema elimu ya ujasiriamali imekuwa na msaada mkubwa kwa makundi maalumu katika kufanya shughuli zao kwa ufasaha, tofauti na wale ambao hawana elimu hiyo ambao wamekuwa wakishindwa kuendelea.

Anasema, wataendelea kujitahidi kutoa elimu ya matumizi sahihi ya fedha za mikopo kabla ya kuvipatia vikundi, na kuwashauri kuanzisha miradi yenye tija ambayo itawanyanyua kiuchumi.

Anafafanua kuwa, vikundi vingi hasa vya vijana na watu wenye ulemavu vimekuwa vikifanya na kushindwa kuendelea, kwa sababu ya ukosefu wa elimu ya ujasiriamali na kuibua miradi yenye tija ambayo itakuwa endelevu.

Anasema halmashauri hiyo imeendelea kutoa fedha za mikopo asilimia 10, nne kwa vijana na wanawake, na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu na kuwataka vijana waendelea kuchangamkia fursa hiyo ili wapate mitaji na kujiajiri wenyewe na kuendesha maisha yao.

Aidha, anataja takwimu ya fedha za mikopo ambayo wameitoa katika Halmashauri hiyo kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, kuwa kwa kipindi cha kuanzia Julai mwaka jana hadi June mwaka huu wametoa Sh. milioni 275.9

"Fedha hizi za mikopo tumezitoa kwa mchanganuo wa vijana a kwa vikundi sita kiasi cha Sh. milioni 148.9, wanawake vikundi nane Sh. milioni 124, kwa walemavu kikundi kimoja Sh 3,000,000"anasema Tesha.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga Beda Chamatata, anaziagiza halmashauri zote mkoani humo kuendela kutoa fedha za mikopo kwa vijana, na kupunguza urasmi wa kuwanyima mikopo hiyo kwa kisingizio kuwa hawarejeshi marejesho kwa wakati, bali waitoe kwao ili wapate shughuli za kufanya na kujiajiri wenyewe.

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Mkulima unapata asali wakati wa ukame, iwapo utayazingatia haya

WAKULIMA wakiwamo wafugaji wanaendelea kusherehekea Sikukuu ya Nanenane, iliyofikia kilele jana, hongereni wakulima, wafugaji wawe wa nyuki, samaki, kamba, wavuvi na kila mmoja anayezalisha ili chakula kiwafikie Watanzania mezani.

Wanapotafakari Nanenane, ukame na uharibifu wa mazingira unatajwa kutikisa ufugaji nyuki, wakulima wanataja uhaba wa maua ya chavua, kukosekana uoto wa asili, nyuki kukosa nguvu na kuanguka ovyo, yote yakichangia upungufu wa asali.

Ukame unapunguza kiasi wanachovuna kutoka madumu 50 yenye kilo 25 za asali hadi chini ya kiwango hicho, anasema Nuru Mwiru, kutoka Kijiji cha Ntonge, kilichoko Manispaa ya Singida.

Nuru akiwakilisha hisia za wenzake wa Jukwaa la Wakulima Wadogo Wanawake maarufu Sauti ya Pamoja ya Wanawake (SAPAWA), Singida DC, ambao pamoja na kilimo pia hufuga nyuki, na kujiongeza kiuchumi anasema mwaka huu una asali haba.

"Nimepata kiasi kidogo, ni chini ya madumu 40 wakati nilifikisha hata zaidi ya madumu 50, kila moja lina lita 25 ni karibu tani nzima ya asali, takribani kilo 750," anasema Nuru na kwamba wanawake wafuga nyuki wengine wameathirika pia.

Anakumbusha kuwa pasipo kulinda mazingira, uoto wa asili na vyanzo vya maji uzalishaji wa asali unakuwa hatarini na kwamba mavuno kidogo linaweza kuwa tatizo la Singida na Dodoma pia.

Ukame umesababisha nyuki kukosa maua mfano kwenye mashamba ya alizeti na kutegemea miti mchanganyiko ya asili mfano miyombo, korosho na maembe na uchavushaji kupitia uoto wa asili ulikuwa mdogo.

Anasema, kuna magonjwa kwa mfano asubuhi wanakuta nyuki wamedondoka na wamekufa, lakini pia hawasafiri kwenda mbali, wanabaikia eneo moja na wakati mwingine mizinga ni myeupe haina asali.

"Tunawaamsha kwa kuwafunika na majani ya mirumbasha (kivumbasi) ili kuwavutia na harufu ya majani hayo." Anasema Nuru.

Mtaalamu wa nyuki, Dk. Felician Kilahama, aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, anazungumza na Nipashe, kuhusu uzalishaji asali na jinsi ukame na mvua vinavyoweza kukwamisha na jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo, zinazowakabili kina mama wakulima.



#### MVUA NYINGI

Anasema mvua ikizidi huondoa chavua kwenye maua na kupukutisha maua hivyo, nyuki hukosa chakula cha kutosheleza mahitaji yao na ya kutengeneza asali ya ziada kwa ajili ya binadamu.

Anasema:"Nyuki wengi huchavusha kwenye mimea midogo (herbs), hivyo mvua ikizidi hujaza maji katika maeneo mengi na kusababisha mimea midogo anayotoa maua kutostawi, hivyo, kuathiri upatikanaji wa maua ambayo nyuki hupata chavua kutengeneza asali. Matokeo yake ni asali kuwa kidogo sana, ambacho ni chakula cha nyuki, anaongeza."

Kadhalika, Dk. Kilahama, anasema mvua ikiwa nyingi huathiri nyuki wafanyakazi kwenda kutafuta chakula, wakati inaponyesha hujifungia ndani. Vilevile, wakati ikinyesha joto la nje ya mzinga hupungua, hivyo kuathiri joto la ndani na nyuki hulazimika kubakia ndani ya mzinga kwa ajili ya kutengeneza joto ili kumlinda malkia.

Aidha, anasema katika misitu au maeneo yenye uoto wa asili ambapo wafuga nyuki hufanyia shughuli zao, sehemu ambayo hata wafugaji huchunga mifugo yao katika maeneo hayohayo, hususani ni majira ya ukame.

Baadhi ya wafugaji hukata miti ovyo kwa nia ya kuboresha malisho ili kupata nyasi zaidi na wakati mwingine kufukuza mbun'go au kutaka kuona mbali kama njia ya kijihami na maadui pamoja na wanyama wakali.

"Wakifanya hivyo miti yenye maua ya kuvutia nyuki hutoweka haraka na nyuki pia.Ukame nao unaathiri ukuaji wa mimea hivyo, inashindwa kutoa maua mengi na yenye afya ambayo yangetoa chavua ambayo nyuki huitumia kutengeneza asali na mazao mengineyo kama nta au 'propolis'."

Anataja tabia ya baadhi ya watu vijijini kuchoma moto hovyo na kuathiri sehemu za kufugia nyuki hata kama wafugaji wangepata asali nyingi, wanaondoka patupu kutokana na athari za moto kwa nyuki.

#### ATHARI ZA UKAME

Ukame unaathiri mimea mingi inayotoa chavua, inatoweka na kuwafanya nyuki wafanyakazi kutumia muda mrefu kwenda kutafuta chamvua kwa ajili ya kutengeneza asali ambayo ni chakula chao na wanadamu pia. Unaweza kusema binadamu ni wezi kwa nyuki, wanamwibia nyuki chakula, anasema Dk. Kilahama.

> Inaweza kuwa vigumu kuwalisha kutokana na ufugaji nyuki tunaotumia kuwa wa kiasili hatujajikita kwenye ufugaji wa kisasa au contemporary beekeeping schemes.

Aidha, maji ambayo ni muhimu yanakuwa ya shida wakati wa ukame ni ya muhimu katika manzuki au apiary au shamba la nyuki. Hivyo, yakikosekana hufanya nyuki wafanyakazi kusafiri umbali mrefu kutafuta maji kwa ajili ya kupooza miili yao hasa joto likiwa kubwa. Lakini pia kwa ajili ya kutenegeneza chakula. Hivyo, wakati wa ukame asali huwa haba, kutokana na upungufu mkubwa wa maji katika maeneo yenye nyuki, anasema.

Cha kufanya ili nyuki wazalishe asali wakati wa ukame ni kutafuta maji na kuyaweka karibu na mizinga, unaweka maji kwenye ndoo au beseni lakini ndani unaweka miti ili nyuki wasidumbukie kwa maana hawezi kuogelea, maji yawekwe kila siku kama unaweka kidogo kwa matumizi ya nyuki .

Vilevile, kuwaandalia chakula kama pumba za mahindi kwa kuyamwaga karibu na mzinga. Kikubwa ni kuandaa chakula na maji na kukiweka karibu na mzinga, nyuki hawatahangaika kwenda mbali kutafuta chakula.

Hatua hii inafaa kwenye wafugaji wenye mizinga ya kisasa na ipo katika kitalu kimoja au kadhaa na havipo mbali sana, kwa mantiki hiyo, mfuga nyuki anaweza kutumia manzuki (shamba la nyuki ) yakawa na afya njema kwa faida ya wote

"Inaweza kuwa vigumu kuwalisha kutokana na ufugaji nyuki tunaotumia kuwa wa kiasili hatujajikita kwenye ufugaji wa kisasa au contemporary beekeeping schemes."

"Baadhi ya changamoto zinazokwamisha hili ni bajeti masuala ya nyuki kuwa finyu, wataalamu wabobezi wachache vilevile, hali za wafugaji vijijini bado ni duni hawajaweza kutengeneza mizinga ya kisasa ya kutosha kati ya 25 hadi 50 kwa kila mfugaji na hatimaye kuanziasha kitalu cha nyuki (bee-Apiary) toshelezi ni kazi kubwa sana."

Ikifikiwa hali kama hiyo itakuwa rahisi kuhudumia nyuki hata wakati wa ukame na kuhakikisha maji yanakuwapo na pia kuweza kuzuia wanyama na wadudu waharibifu wasilete madhara kwenye mizinga ya nyuki.

# Fahamu 'matangi' yanavyotunza maji

INATOKA UK.11

misitu katika Milima ya Uluguru na Udzungwa ilikuwa minene, ilihifadhi maji mengi ya mvua.


Viashiria vilionyesha kuwa katika kipindi hicho mito ilikuwa na maji mengi kwa mwaka mzima. Kwa upande wa Mto Ruvu, ambao unaanzia katika misitu ya Milima Uluguru haukuwa na changamoto nyingi za maji kama ilivyo sasa.

Vilevile, mito yenye vyanzo vyake katika misitu iliyofunika Milima ya Udzungwa (Kilombero, Kihansi na Ruaha ilijaa maji mengi. Hali hiyo, ilitokana na misitu kutoharibiwa na shughuli mbalimbali za kibinadamu.

Wakati huo kulikwepo na kada ya walinzi misitu (forest guards/ rangers). Kupitia ulinzi madhubuti uliokuwepo, uharibifu wa misitu ulikuwa kwa kiwango cha chini sana na rasimali hiyo ilistawi.

Ulinzi huo ulineemesha misitulindi maji (Kenya huita 'water towers') na ikawa na afya nzuri kiasi kwamba chini yake kulikuwa na mimea midogo midogo mingi, majani, matawi na miti iliyokuwa ikizeeka au kufa ilianguka na kuzidi kurutubisha ardhi.

Miti hiyo ilitengeneza tabaka kubwa misili ya sponji lililojaa maji, majani, mizizi miti iliyooza na kulifanya eneo hilo kuwa hali ya umajimaji uliostawisha viumbe vya kila aina huku maji yakituama. Hivyo, mvua ikinyesha asilimia 90 ya maji ya mvua yalikuwa yakihifadhiwa msituni.



Sehemu hizi ni 'matangi ya asili' yanayohifadhi maji yanayopatikana maeneo mbalimbali. **PICHA: MTANDAO**

Uchomaji moto kwenye maeneo hayo ulikuwa nadra na usingeunguza eneo kubwa kutokana na ubichi mwingi misituni Uluguru ilikuwa inatiririsha maji mwaka mzima.

Baadhi ya vijito vilitiririsha maji miaka ya 1974 hadi 1977 wakati nikiwa chuo kikuu nasoma shahada ya kwanza ya taaluma ya misitu, katika Kitivo cha Kilimo, Mifugo na Misitu cha Chuo Kikuu cha Dar-Es-Salaam,mjini Morogoro, tulishuhudia misitu milimani imefunikwa na mawingu mwaka mzima. Ilikuwa shida kuona jua huko mpaka kukawapo na sehemu inaitwa 'morning-site' ambako jua lilikuwa likioneka kuanzia saa 9 hadi 10 alasiri.

Wakati huohuo, maji yakitiririka milimani mwaka mzima mpaka mwanamuziki Mbaraka Mwishehe, sasa ni marehemu, akatunga wimbo kusifia mandhari nzuri katika Milima ya Uluguru.

"Maji yanatiririka milimani oyee" aliimba Mwishehe. Lakini sasa hayaonekani tena yamekauka. Siyo jambo jema ni hatari kwa taifa bila kujali wewe unaishi Morogoro au Manyara.

Matangi hayo yalihifadhi maji na kuwezesha Tanzania nzima kupata mvua na nchi kubarikiwa kwa vyakula, hali ya hewa bora, wanyama na mimema mbalimbali ikastawi. Ni lazima kuchukua hatua.

Katika misitu ya Uduzungwa maporomoko ya maji yalikuwa makubwa kuliko sasa na vijito vilikuwa vingi. Mwaka 2017, baada ya kuvuka daraja Mto Ruaha kuelekea Ifakara mjini, nilihesabu vijito 32 vilivyokuwa vinatoka msituni kupeleka maji katika bonde kutumika katika umwagiliaji, mpunga na miwa.

Hata hivyo, maji yake yalikuwa yamepungua sana ukilinganisha na miaka ya nyuma wakati misitu ikiwa na hali ya kupendeza. Mto Ruaha Mkuu ulikuwa ukisheheni maji mengi mwaka mzima. Lakini sasa ni shida ukifika wakati wa kiangazi hauna maji ya kutosha kiasi cha kuhatarisha uhai wa wanyamapori katika mbuga ya Ruaha, yote hayo yakitishia uhai wa sekta ya utalii.

Siku hizi kilimo cha mpunga katika maeneo ya wilaya ya Mbarali pia kimekuwa cha kusuasua kutokana na upungufu mkubwa wa maji. Lakini baada ya miaka 1970 hadi 80 serikali kufuatia kada hiyo ya walinzi wa misitu, misitu ya asili imekosa ulinzi ipasavyo na sasa ukame unatikisha taifa.

Kila mkoa changamoto ni kuhangaika na maji pamoja na athari kuwa kubwa zaidi kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Katika toleo linalofuata makala itachambua athari zinazotokana na uharibifu wa misitu kwa sekta ya maji pia na sekta nyingine kuashiria kwamba misitu ni sekta mtambuka na muhimu ambayo inahitaji ulinzi na watu kuelimishwa ulazima wa kuiogopa na kuitunza.

## WANENAVYO MALENGA

### VITU LAINI LAINI

Watu wengi siku hizi, hukwepa vitu vigumu,
Wanakacha zile kazi, wazionazo ni ngumu,
Wanakwepa utatuzi, hata yaliyo muhimu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Hata kama ni chakula, hukwepa kile kigumu,
Ugali kwa shida wala, ila chipsi ni tamu,
Ule unalimwa Kyela, wabugia bila zamu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Kazi ya shamba kulima, kwa uchumi ni adhimu,
Kila mtu anasoma, kwingine akajikimu,
Kubeti wanajituma, kwa sababu pesa tamu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Watu wanasema sana, tadhani ni watalamu,
Sasa na wao kutana, ikibidi kama timu,
Pamoja mkiungana, kuandika kwa kalamu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Kuku mifupa mifupa, zama zile nyama tamu,
Unashika lako fupa, tafuna iishe hamu,
Sasa sawa na kukopa, minofu ndiyo mitamu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Changamoto zaibuka, ni kulaumulaumu,
Badala kuwajibika, kwenda mbali wajihimu,
Baadaye wakifika, wazidi kucheza gemu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Watu wanapewa miwa, juisi yake ni tamu,
Ila kutafuna miwa, meno yao ni vigumu,
Visu ndiyo hutumiwa, acha meno yale sumu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Ule wimbo dezo dezo, muda wake umetimu,
Watu wenye uwezo, waja watu kukaimu,
Umri kwao uozo, hao wengi wamo humu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Wanachopenda kulishwa, hata matunda damu,
Ikibidi kuvalishwa, waume kama mademu,
Ni kama wameloweshwa, na kukosa ufahamu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Ili uwe ni mshindi, upambane na magumu,
Huja vipindivipindi, sawasawa na swaumu,
Na wewe jaza ufundi, mwishowe utahitimu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### NYIE VIONGOZI WETU

Washuhudie foleni, ili watutatulie,
Tuwe nao mitaani, vibaka wawaibie,
Pesa zao mfukoni, mafuta wanunulie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Sisi tujichagulie, na viti wavikalie,
Na halafu tusalie, mengi tulalamikie,
Wenyewe tuangalie, keki yetu wajilie,
Hapo matatizo yetu, hatupati utatuzi.

Yale tunayapitia, na wao wayapitie,
Pale tunapoumia, pia wao waumie,
Ndipo watapoanzia, yote washughulikie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Muda wao wa kula, hilo tusilisikie,
Ni kazi bila kulala, hiyo kwao tusikie,
Hii ya kwetu misala, na wao iwafikie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Sisemei huku kwetu, nitaje unisikie?
Hili hili bara letu, hebu tuliangalie,
Hawa viongozi wetu, ili tuwafurahie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Kabla zetu chaguzi, tuliko watufikie,
Hata kama twala ndizi, na wao tuwagawie,
Hata makundi sogozi, humo nao waingie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Ukitoka kijiweni, zao kura wapatie,
Washinde wawe enzini, jaribu uwafikie,
Ni kama madhabahuni, si rahisi ufikie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Hujamchagua wako, ili akutumikie,
Kura zako za mashiko, kitiche akikalie,
Ni kudra kwako, jaribisha umwingie,
Hapo matatizo yetu, hayapati utatuzi.

Afrika tuamke, tusibaki tusinzie,
Viongozi tuwapike, sisi watutumikie,
Nasi nafasi tushike, kazi tusijivunie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Nyie viongozi wetu, pongezi ziwafikie,
Mnaojali ya kwetu, acha tuwashangilie,
Ziko vema kura zetu, bora tujifagilie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Watahadharishwa ununuzi dawa za mifugo holela

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAFUGAJI wametakiwa kuacha kununua dawa za mifugo kiholela kwenye minada na magulio ili kijiepusha kuuziwa dawa zisizo na ubora na kuhatarisha afya za walaji.

Meneja Kanda ya Kati wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Sonia Mkumbwa, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akitoa elimu kwa wafugaji waliotembelea banda la mamlaka hiyo kwenye maonesho ya Nanenane jijini hapo.

Alisema wafugaji hao wanapaswa kujiepusha na ununuaji holela wa dawa hizo kwenye minada na magulio kwa kuwa hazijakidhi ubora, usalama na ufanisi.

Aidha, Mkumbwa alisema TMDA ina jukumu la kuhakikisha kuwa bidhaa za dawa zikiwamo za mifugo, vifaa tiba na vitendanishi vina ubora kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kimataifa na kitaifa ili kuendelea kumlinda mwananchi.

"TMDA inahakikisha inafuatilia ubora wa bidhaa hizo mara kwa mara katika soko kwa kufanya kaguzi katika maeneo ya kuzalishia, kutunzia na kuuzia ili kuhakikisha matokeo yaliyoko katika soko yanakidhi vigezo ikiwapo kufanya uchunguzi wa kimaabara."

"Maabara yetu imethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na endapo mamlaka itabaini kuna bidhaa zisizo na ubora, hatua za kisheria huchukuliwa kwa waliokiuka ikiwamo uteketezaji wa bidhaa hizo pamoja na tozo za faini kwa mujibu wa sheria," alisema.

Vile vile, alisema TMDA inaendelea kufuatilia usalama wa bidhaa inazodhibiti na kuwataka wananchi kutoa taarifa endapo watapata madhara yoyote kutokana na matumizi ya bidhaa hizo.

**Alisema wafugaji hao wanapaswa kujiepusha na ununuaji holela wa dawa hizo kwenye minada na magulio kwa kuwa hazijakidhi ubora, usalama na ufanisi.**

# Wanaume washauriwa kusimamia wake zao unyonyeshaji watoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAUME wametakiwa kuwashauri na kuwasimamia wake zao wanyonyeshe ipasavyo watoto ili kuondokana na udumavu wa akili.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Huduma na Lishe wa Wizara ya Afya, Dk. Grace Mosha, aliyasema hayo juzi jijini hapo kwenye semina ya waandishi wa habari ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Unyonyeshaji.

Alisema wakati mwingine wanawake wanashindwa kunyonyesha ipasavyo watoto ili matiti yao yasilale kuwafurahisha waume zao jambo ambalo linasababisha udumavu kwa watoto.

"Mnyonyeshe mtoto wako ipasavyo, suala la kukwepa matiti kulala, unamkosesha mwanao maziwa yatakayomfanya asiwe na udumavu wa akili, sasa wewe unaacha kumnyonyesha mtoto unamwangalia mwanaume badala umwangalie mtoto, maziwa ya mama ni muhimu sana kwenye ukuaji wa mtoto."

"Hata wale ambao wananyonyesha na kujikuta tayari wamebeba mimba nyingine hawapaswi kuwaachisha kunyonya watoto, wanatakiwa kuhakikisha mtoto ananyonya hadi umri anaostahili kuachishwa, nyonyesha tu hata mimba ikifika miezi tisa angalau utakuwa umemsogeza huyu kwenye umri ambao anastahili kuliko kumkatisha," alisema.

Aliwaasa waandishi wa habari kutoa elimu kwa jamii ili kusaidia watoto kunyonyeshwa ipasavyo hadi watimize miaka miwili au zaidi.

Naye Ofisa Lishe, Herieth Lumanyika, alisema takwimu zinaonesha watoto wanaoanzishwa kunyonya maziwa ya mama ndani ya saa moja baada ya kujifungua ni asilimia 53.5.

"Watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama pekee kwa kipindi cha miezi sita asilimia 58, watoto wanaoendelea kunyonyeshwa hadi kufika umri wa mwaka mmoja ni asilimia 92.2, wanaonyonyeshwa hadi kufika miaka miwili ni asilimia 43, mnaona ambavyo inazidi kushuka, tunashauri mtoto anyonyeshwe maziwa ya mama hadi miaka miwili au zaidi, lakini wengi wanaishia katikati hawafiki," alisema.

Alisema mtoto anatakiwa kunyonya hadi miaka miwili ili kutimiza siku 1,000 za ukuaji wake.

"Watoto wanaoanzishwa vyakula vya nyongeza katika umri sahihi ni asilimia 87, wanaopatiwa mlo kamili wenye mchanganyiko wa makundi sahihi ya vyakula ni asilimia 35, hapa pia tuna changamoto, mtoto anapoanza kula vyakula vya ziada, wazazi wengi hawajapata elimu ya mlo kamili, wengine wanadhani chakula kinachomfaa mtoto ni uji, sio sawa na wengine wanahita uji lishe, lakini ukiangalia umejaa nafaka tu," alisema.

Alisema watoto wengi hawapati mchanganyiko sahihi wa makundi ya vyakula huku watoto wenye umri wa miezi sita hadi 23 wanaopewa mlo bora ni asilimia 30.

Mtaalamu huyo alisema endapo mtoto atanyonyeshwa vizuri itamsaidia ukuaji wa mwili na akili na kuondokana na tatizo la utapiamlo.

"Kasi ya watoto kupata magonjwa ya kuambukiza itapungua na vifo vya watoto nchini vitapungua, lakini kwa wanawake faida ya kunyonyesha ni kupunguza uwezekano wa kupata saratani ya matiti na via vya uzazi," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Lishe, Jenipher Mayenga, alishauri kinamama kujiepusha na matumizi ya chupa za kulishia watoto ili wasipate magonjwa na kuharibu mfumo wa chakula.

"Kumlishia mtoto kuna madhara pia inachangia mtoto kupaliwa sana na akipaliwa mara kwa mara inaathiri mfumo wake wa chakula na hewa," alitahadharisha.

Hata hivyo, alisema kutokumnyonyesha mtoto mara kwa mara kunachangia uzalishaji wa maziwa kuwa kidogo.

"Kumnyonyesha mtoto titi moja kwa muda mfupi kunasababisha kusiwe na uzalishaji mzuri wa maziwa, lakini msongo wa mawazo unasababisha pia uzalishaji kuwa mdogo kwa kuwa huathiri homoni zenye jukumu la kuzalisha maziwa ya mtoto," alisema.



Kaimu Ofisa Mfawidhi wa Makazi ya Wazee Njoro Moshi mkoani Kilimanjaro, Christa Katorogo, akitoa taarifa ya makazi hayo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula (hayupo pichani), juzi. Katibu yuko katika ziara ya kutembelea makazi ya wazee kwenye maeneo mbalimbali nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi waishukuru serikali kuwajengea zahanati

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

WANANCHI wa Kijiji cha Nagulo, Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, wameishukuru serikali kwa kuwajengea zahanati ambayo haikuwapo tangu kuanzishwa kwa kijiji hicho.

Mwavulla Mathayo akizungumza na waandishi wa habari kijijini hapo jana, alisema walikuwa wakilazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya na wakati mwingine kuishia kutumia miti shamba kutokana na umbali huo.

"Tuna kila sababu ya kumshukuru kwa serikali yetu kwa kutupatia zahanati hii, sasa tutaweza kuachana pia na kutumia dawa za miti shamba na pia itatuondolea kero ya kutembea mwendo mrefu kufuata matibabu," alisema.

Naye Morine Makasi, alisema zahanati hiyo ni mkombozi kwa kuwa itaokoa gharama za kwenda kutafuta huduma za afya Bahi Mjini.

"Kuna wakati mjamzito anatembea umbali mrefu kufuata huduma za kliniki na kujifungua na hii ilikuwa inasababisha wengine kujifungulia nyumbani, tunashukuru serikali na mbunge wetu (Kenneth Nollo) kwa kutusogezea huduma hii muhimu," alisema.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Bahi, Agustino Ndonu, alisema kuwa ujenzi wa zahanati hiyo unatarajiwa kukamilika hivi karibuni na utaondoa adha ya wananchi waliokuwa wakitembea umbali wa kilomita 17 kufuata huduma za afya.

"Ujenzi upo hatua za umaliziaji na utakapokamilika utawapunguzia adha wananchi kutembea umbali wa kilometa 17 kufuata huduma Bahi Mjini au Kitinku, Wilaya ya Manyoni mkoani Singida na Dodoma mjini," alisema.

Alisema, zahanati hiyo itakapokamilika iatatoa huduma kwa wananchi 10,000.

Alifafanua kuwa fedha za ujenzi wa zahanati hiyo ni Sh. milioni 100 na kati ya hizo Sh. milioni 50 zikitoka kwa Halmashauri ya Bahi, Mfuko wa Jimbo, Shilingi milioni sita na wananchi wamechangia nguvu kama kubeba mchanga na mawe.



# Bil. 27/- kujenga maghala maeneo ya uzalishaji

**Na Renatha Msungu,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, amesema wizara hiyo inatarajia kutumia Sh. bilioni 27 kwa ajili ya kujenga maghala katika maeneo ya uzalishaji huku akisisitiza namna ya kukopesha wakulima kwa bei nafuu.

Hayo yalibainishwa jijini hapo katika kongamano la shamba darasa lililoandaliwa na wizara hiyo kwenye maonesho ya Nanenane yanayoendelea jijini hapo.

Alisema kwa kuanzia wataanza na maghala 70 katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha yanakuwapo kwa ajili ya kuhifadhia chakula.

Alisema katika Ajenda ya 10/30 inatakiwa ifikapo 2030 kilimo kiwe kinachangia kwa asilimia 100 kwenye Pato la Taifa.

"Serikali imejipanga kuhakikisha fedha hizo zinatolewa hivyo wakulima wachangamkie fursa hiyo," alisema Mavunde.

Alisema jitihada za serikali ni kubwa katika kuhakikisha inajenga maghala hayo ambayo yatasaidia katika kuhifadhi chakula.

Mavunde ameongeza kuwa serikali ina tatizo la mafuta ya kula na inatumia Sh. bilion 470 kuingiza mafuta hayo na uhitaji ni tani 650,000 wakati nchi inazalisha tani 250,000 hadi 300,000 na kueleza kuwa inapaswa kuongeza uzalishaji kwenye zao la alizeti.

"Tunakaribisha wawekezaji wakubwa kuja kuwekeza tuondokane na kilimo cha ekari moja moja na twende tukawekeze kwenye mashamba makubwa," alisema Naibu Waziri huyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Goeffrey Mkamilo, alisema wana aina za mbegu 380 katika mazao mbalimbali na kwamba ifikapo Juni 30, 2023, watakuwa wamefikia aina za mbegu 400.

Alisema kwa kutumia mbegu bora zenye ukinzani na magonjwa ambazo zimehakikiwa na wizara, tija inaongezeka kutoka tani 10, hadi 70.

Mkurugenzi huyo alisema wanatarajia kuzalisha tani 1,400 za mbegu ambazo ni za daraja la awali la msingi ifikapo Juni 30, 2023.

Hata hivyo, alisema lengo la kuzalisha mbegu hizo ni kuwapatia Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), ili kuzihakiki na kuwafikishia wakulima.

Awali, Mshauri wa Sera za Kilimo, Prof. David Nyange, alisema kuna vitu vitatu ili kufikia malengo yenye tija kwenye kilimo ambayo ni mbegu bora, miundombinu bora ya nishati na lishe kwenye mazao ambayo ni afya ya udongo.

Naye Mkurugenzi wa Takwimu za Kiuchumi kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania (NBS), Daniel Masolwa, alisema sera na mipango ya serikali ipo wazi na Agosti 23, mwaka huu kuna Sensa ya Watu na Makazi.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Asas Group, Ahmed Salim Asas akitoa maelezo kwa Rais Samia Suluhu Hassan alipotembelea banda la Asas Group kwenye maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika kitaifa jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi mikoa waaswa kutumia fursa za utalii

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amewaasa viongozi wa mikoa, wilaya na halmashauri kutumia fursa za utalii zilizofunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kupitia filamu ya Royal Tour kuhamasisha utalii katika maeneo yao.

Waziri Dk. Kijaji aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati wa uzinduzi wa Filamu ya The Royal Tour Nyanda za Juu Kusini ambayo iliambatana na uzinduzi wa Makala ya Vivutio vya Utalii vinavyopatikana katika mikoa iliyoko Nyanda za Juu Kusini.

Dk. Kijaji alisema serikali imetumia nguvu kubwa kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii vilivyoko Tanzania na ni wajibu wa kila kiongozi na mwananchi mmoja mmoja kuunga mkono juhudi hizo kwa kuendelea kuhamasisha utalii.

Dk. Kijaji alifafanua kuwa Tanzania kupitia filamu ya 'The Royal Tour' imeweka lengo la kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vivutio vya utalii kutoka milioni 1.5 hadi kufikia milioni tano na mapato kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 hadi bilioni sita ifikapo mwaka 2025. Kufuatia lengo hilo Dk. Kijaji alitoa wito kwa wadau wa utalii waongeze kasi katika kuhamasisha na kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema tayari wameanza jitihada za kuvitangaza vivutio mbalimbali vya utalii vinavyopatikana mkoani humo.

Alisema, wadau kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa mkoa waliandaa kitabu kinachoelezea fursa mbalimbali za uwekezaji na utalii vinavyopatikana na tayari wawekezaji wameanza kujenga miundombinu ya hoteli za kisasa kwa ajili ya watalii na wageni.

# Watakaokaidi kutumia tiketi kimtandao mabasi yao kufungiwa

**Na Renatha Msungu** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesema itawachukulia hatua kali wamiliki wa mabasi watakaokaidi kuingiza mabasi kwenye mfumo wa ukataji tiketi kwa njia ya mtandao ifikapo Agosti 30, mwaka huu.

Aidha, mamlaka hiyo imesema hadi kufikia jana tiketi zilizouzwa kwa njia ya mtandao (E ticket) zilikuwa 9,728.

Akizungumza na waandishi habari jana katika maonesho ya kitaifa ya Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya John Mwakangale, Mkurugenzi wa Usalama Barabarani Johansen Kahatano, alisema moja ya hatua ambazo zitachukuliwa dhidi yao ni pamoja na mabasi kufungiwa, kupigwa faini pamoja na kushusha abiria kama watakutwa barabarani wamepakia ili hali hawapo kwenye mfumo huo.

Alisema wamiliki wa vyombo vya usafiri barabarani wanapaswa kusajili mabasi yao kwenye mfumo kabla ya tarehe ya mwisho ya kusajili iliotangazwa.

"Nawaomba wamiliki wa mabasi kusajili mabasi yenu katika mfumo, mahitaji kuona kila basi lipo kwenye mfumo ili kuepuka kufungiwa," alisema Kahatano.

Alisema wenye mabasi wakifanya hivyo itasaidia kujua usalama wa magari barabarani ikiwamo kuona kama yanakwenda kinyume na mwendo uliopangwa yanapokuwa katika safari zao za kila siku.

Aidha, alisema idadi ya mabasi nchi nzima ni 7,500, lakini yanayofanya kazi kila siku ni machache na kutoa mfano mabasi yaliyotoka jana kwenye mfumo ni 4,500.

Akizungumzia mfumo wa E ticket alisema hadi jana zilizouzwa kwa mtandao ni 9,728 huku akisisitiza jamii idai E ticket pale inapofika kwenye ofisi kwa ajili ya kukata tiketi ya safari.

"Naomba jamii ijenge utaratibu wa kuomba E ticket pale wanapokuwa wanauhitaji wa tiketi za safari," alisema Kahatano.

Alisema kila mwananchi anahitaji kukata hiyo ili kuepuka msongamano katika ofisi za ukatishai tiketi.

Naye Erasto Mwansasu, alisema mfumo huo ni mzuri kutokana na kusaidia kupunguza usumbufu unaojitokeza katika ukataji tiketi.

Alisema ukienda katika ofisi ambazo hawatumii mfumo huo kuna msongamano.



## ‘Wanawake, vijana washirikishwe utoaji haki’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya wa Kati Unguja, Marina Joel Thomas, amezitaka kamati za ulinzi na usalama katika ngazi zote za shehia, wilaya na mkoa kuwashirikisha wanawake na vijana katika utoaji wa maamuzi kwenye utatuzi wa migogoro ili kuepusha uvunjifu wa amani nchini.

Akifungua mafunzo jana yaliyoandaliwa na Taasisi ya Zanzibar Gender Coalition, Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja, alisema wanawake na vijana wana nafasi kubwa ya kudumisha amani na kuwataka washirikishwe katika kila nyanja ili kuleta usawa wa utoaji wa haki ambayo ni kichocheo cha kudumisha amani nchini.

Hata hivyo, alizitaka asasi za kiraia kuendelea kushirikiana na serikali katika mambo muhimu ya kukuza maendeleo hasa la uhamasishaji wa amani na utulivu katika nchi.

Marina aliwataka wananchi kuzifuata sheria za nchi zilizowekwa kwenye ngazi zote hata zile za shehia ili kuepuka kuingia katika migogoro ambayo italeta mifarakano na kuchangia kuvunjika kwa amani ya nchi.

Akiwasilisha mada ya umuhimu wa kuwapo amani, Asha Aboud Mzee, alisema jukumu la kulinda amani ni la watu wote ni lazima washirikiane katika utoaji wa elimu kuhamasisha wananchi kuacha vitendo vitakavyohatarisha amani ya nchi.

Aboud alisema, amani na utulivu ndiyo inayozaa maendeleo katika nchi na endapo ikitoweka itasababisha athari kubwa ikiwamo vita vya wenyewe kwa wenyewe, migogoro, uchumi wa nchi kushuka na kushindwa kuzalisha huduma bora kwa wananchi wake.

Alisema Zanzibar ipo amani ya kutosha ndiyo maana serikali inaendelea kupiga hatua katika nyanja za maendeleo ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, shule, soko na mambo mengine ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Kwa upande wao washiriki wa mafunzo hayo wakiwamo Masheha, Wasaidizi wa Sheria, wanaharakati wa udhalilishaji, baraza la vijana na watendaji wa halmashauri wameiomba serikali kukaa chini na wananchi wake katika kuitafutia ufumbuzi migogoro ya upatikanaji wa haki pamoja na huduma muhimu za jamii ili kukinga uvunjifu wa amani nchini.

Kwa upande wao wawakilishi kutoka Taasisi zisizo za kiserikali Zanzibar (Gender Coalition), Mwandawa Khamis na Neil Ngala kutoka Foundation for Civil Society, walisema amani ikitoweka katika nchi waathirika wakubwa ni wanawake na watoto pamoja na watu wenye ulemavu na kwamba serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii pamoja na kufanya utatuzi wa mambo yanayolalamikiwa na wananchi ili kwenda sawa katika uimarishaji wa maendeleo. Walisema wanaharakati mbalimbali wa maendeleo wapo mstari wa mbele kuisaidia serikali kwenye uhamasishaji wa amani kwa jamii, lakini malalamiko yanayoibuliwa yafanyiwe kazi kwa haraka ili kuleta mabadiliko na vijana ndiyo wanaongoza vurugu.

Naye Mwenyekiti wa JUWAUZA akiwasilisha mada ya utatuzi wa migogoro, Salma Saadat, alisema migogoro mikubwa iliyokuwapo Zanzibar ni ya kiutawala ambao ni wa kisiasa, kitabaka ni udini na ukabila, kijamii ambayo ni ndoa, mirathi, malezi na mgogoro wa kiuchumi ambao ni rasilimali, mipaka, misitu na isipo fanyiwa kazi ya utatuzi kwa haraka utaleta athari kubwa katika nchi.

Aidha, aliiomba serikali kuwapa wanawake nafasi katika usuluhishi wa migogoro katika jamii ambayo itasaidia upatikanaji wa amani na utulivu wa nchi.

# Mradi barabara kuimarisha sekta ya usafiri, utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Dk. Khalid Salum Mohamed, amesema utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 100.94 utaimarisha sekta ya usafiri na kukuza utalii ikiwamo maeneo ya Mji Mkongwe.

Aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar wakati akitoa ufafanuzi wa utiaji wa saini wa mradi wa ujenzi wa barabara za mjini.

Alisema ujenzi wa barabara za ndani na barabara kuu ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ya Zanzibar ili miundombinu kuimarishwa na kufungua fursa za kiuchumi na maendeleo.

Alisema zaidi ya miaka 50, serikali haijafanya matengenezo ya maana ya barabara za mjini na kusababisha usumbufu mkubwa na kurudisha nyuma juhudi na mikakati ya kuimarisha sekta ya utalii.

Alisema ukuaji wa uchumi wa nchi kiasi kikubwa unategemea kuwapo kwa miundombinu imara ya barabara ambazo zitasaidia shughuli za usafiri na sekta ya utalii.

Alisema uharibifu wa barabara za ndani unaisababishia serikali kuingia gharama za Sh. bilioni 15 kila mwaka kwa ajili ya matengenezo baada ya kumalizika kwa mvua za masika.

“Mradi wa ujenzi wa barabara za ndani za mji ni muhimu ambao utasaidia huduma za usafiri pamoja na kukuza utalii na kuongeza uchumi wa nchi,” alisema.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Khadija Rajab, alisema mradi huo unahusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 100.94 ambao unatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu.

Alisema ujenzi huo pia utahusisha njia za barabara za juu (Flyover) mbili zinazounganisha makutano ya Barabara ya Amani hadi Mwanakwerekwe ambazo kwa kiasi kikubwa zitapunguza msongamano uliopo sasa kutokana na kuongezeka kwa shughuli za wananchi kiuchumi na kijamii.

Alisema ujenzi wa barabara za ndani utasaidia na kutoa ajira za vijana wapatao 100 watakaofanya kazi katika maeneo mbalimbali.

“Ujenzi wa barabara za ndani ni wa miaka mitatu ambao utahusisha barabara zenye urefu wa kilomita 100.94 pamoja na barabara za juu Fly over mbili zinazounganisha barabara ya Amani pamoja na Mwanakwerekwe,” alisema.

Rajab alisema mradi wa ujenzi wa barabara za ndani unatekelezwa na kampuni kutoka China ya CCECC ambayo ni miongoni mwa kampuni kubwa yenye uzoefu wa ujenzi wa barabara pamoja na madaraja na njia za reli pamoja na kutekeleza miradi hiyo katika nchi mbalimbali ikiwamo katika Bara la Afrika.

Utiaji wa saini wa ujenzi wa barabara hizo zenye urefu wa kilomita 100.94 ulishuhudiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na kutiwa saini na Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Khadija Rajab, pamoja na Mkurugenzi wa Kampuni ya CCECC kutoka China, Zhang Junle, Ikulu Zanzibar.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Mzee Ali Ameir Mohammed alipofika nyumbani kwake Donge Kichavyani Mkoa wa Kaskazini Unguja, kumjulia hali yake juzi. **PICHA: IKULU**

# Makarani sensa watakiwa kuzingatia weledi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMISAA wa Sensa Zanzibar, Mohammed Haji Hamza, amewataka makarani na wasimamizi TEHAMA na maudhui kuwa weledi na kuzingatia uadilifu wakati wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Aliyasema hayo alipofanya ziara ya kuvitembelea vituo vya mafunzo kwa watendaji hao katika Mkoa wa Kusini Unguja jana.

Alisema uzalendo na uadilifu wakati wa zoezi hilo utasaidia upatikanaji wa takwimu sahihi zitakazoisaidia serikali kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo endelevu ya nchini.

“Tunatakiwa kuhakikisha tunazingatia uadilifu pamoja na weledi wa taifa ili kuyafikia yale ambayo yanakusudiwa kupatikana katika zoezi la sensa,” alisema.

Alisema sensa ni nyeti katika ustawi wa Taifa la Tanzania na wanapaswa kuwa waadilifu na kuzingatia maadili pamoja na kusimamia vizuri kazi hiyo.

Alisema, ni vizuri kuelewa wamebeba dhamana kubwa na majukumu ya serikali ili kuhakikisha inakwenda salama.

Kadhalika, alisema, suala la sensa linalindwa na sheria ili ikitokea karani akaharibu, hatua za kisheria zitachukuwa nafasi yake kwa kuwa sensa ni jukumu ambalo linalindwa na sheria za nchi.

Aidha, alisema mafunzo hayo yatawasaidia makarani kwenda kukusanya taarifa sahihi zitakazosaidia katika mipango ya maendeleo ya taifa na wananchi wake kwa ujumla.

Naye Mratibu wa Sensa Mkoa wa Kusini Unguja, Muhina Khamis Suleiman, alisema tayari wanaendelea na mafunzo ya nadharia na vitendo kwa ajili ya kwenda kuchukua taarifa kwenye kaya na maeneo mengine ikiwamo takwimu za majengo na huduma za jamii kwa ngazi za shehia.

“Kila kitu kinakwenda vizuri kama ilivyopangwa, wanafunzi wanawajibika ipasavyo na wana ari ya kujifunza,” alisema.

Kwa upande wake Mkuu wa kituo cha Mtule, Khamis Rubea Buheti, alisema, watendaji hao wamekuwa wakitoa ushirikiano na ari ya kujenga uelewa wa kinachofundishwa kutoka kwa walimu wao.

# SIKU YA WAKULIMA




Baadhi ya wananchi waliohudhuria Sikukuu ya Wakulima Nanenane katika Viwanja vya John Mwakangale Mbeya jana. **PICHA: IKULU**




Rais Suluhu Hassan akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mfumo wa ruzuku ya mbolea baada ya kutembelea mabanda na kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na wadau wa kilimo katika kilele cha maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane kitaifa ambayo imefanyika katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya. **PICHA: IKULU**



Rais Samia Suluhu Hassan akishuhudia utiaji saini wa makubaliano ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji nchini katika kilele cha maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana. **PICHA: IKULU**



Rais Samia Suluhu Hassan akikabidhi mfano wa funguo za trekta kwa ajili ya wakulima bora ambao wamepewa zawadi kutokana na mafanikio waliopata katika kilimo. **PICHA: IKULU**



Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Waziri wa Kilimo alipotembelea banda la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) na la Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) kwenye kilele cha Sikukuu ya Wakulima Nanenane kitaifa katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana. **PICHA: IKULU**




Ofisa Mauzo wa Kampuni ya GF Trucks & Equipment's ltd, Poul Msuku, akitoa zawadi ya fulana kwa mmoja wa wateja waliotembelea banda lao katika uzinduzi wa gari maalumu Siku ya Wakulima yenye kauli mbiu ya Kilimo Usafishaji katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana. **NAMPIGAPICHA WETU**

HABARI KIMATAIFA

# Leo ni leo Uchaguzi Mkuu Kenya

**Nairobi,** KENYA

LEO Wakenya wanapiga kura kuamua viongozi watakaowaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo katika ngazi ya kitaifa mpaka kaunti.

Viongozi wanaochaguliwa katika uchaguzi huo ni Rais, Wabunge, Seneta, Gavana na Wawakilishi wa kaunti mbalimbali.

Aidha, kwa nafasi ya urais ushindani mkubwa ulioko baina ya mgombea wa Muungano wa Azimio la Umoja One Kenya maarufu Azimio Coalition, Raila Odinga na Naibu Rais William Ruto anayewania kupitia tiketi ya Chama cha United Democratic Alliance (UDA) maarufu Kenya Kwanza Coalition.

Wengine ni Prof. George Wajackoya wa Chama cha Roots na Waure Waohiga wa Chama cha Agano.

**Hapa Bungoma sote tuko salama. Tumeona wasafiri wengi wakipitia hapa wakielekea katika mji wa Busia (mpakani na Uganda) ambako walijiandikisha kama wapigakura.**

Wakati joto la uchaguzi huo likiwa juu, jana wananchi wa nchi hiyo walikusanyika kwenye vituo mbalimbali vya kupigia kura kutafuta kadi ya mpigakura, ili wapate haki ya kikatiba siku ya leo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Tume Huru ya Uchaguzi na mipaka ya majimbo (IEBC), Wakenya milioni 22 wamejiandikisha kupiga kura, huku ikiendelea kusafirisha vifaa vya uchaguzi na kwamba vituo vitafunguliwa saa 12 alfajiri na kufungwa saa 11 jioni.

Aidha, kampuni za usafiri nchini humo zimeshuhudia ongezeko la idadi ya Wakenya wanaokata tiketi dakika za mwisho kwenda kwenye maeneo yao ya uchaguzi, walikutana na ulanguzi wa nauli.

Tathmini ya BBC Magharibi mwa Kenya imegundua kuna mamia ya abiria wanaoharibu kurudi nyumbani kwenye vituo vyao vya kupigia kura walikosajiliwa huku baadhi ya maeneo nauli za mabasi zikiongezeka maradufu kutokana na mahitaji ya watu wengi kutaka kusafiri.

Eneo la Magharibi mwa nchi hiyo lenye jumla ya wapigakura milioni 2.6 wa kwenye kaunti tani, linaonekana kama eneo muhimu kuamua mshindi wa kura ya rais.

"Hapa Bungoma sote tuko salama. Tumeona wasafiri wengi wakipitia hapa wakielekea katika mji wa Busia (mpakani na Uganda) ambako walijiandikisha kama wapigakura," alisema wakala wa usafiri Kennedy Ajimbi.

Katika Mji wa Eldoret, wapigakura pia wamekuwa wakithibitisha kuwa wako kwenye usajili wa mwisho wa uchaguzi.

Katika eneo la Bonde la Ufa nchini Kenya, Eldoret, inaonekana kama ngome ya Naibu Rais William Ruto, ambaye leo atapiga kura katika mji aliozaliwa wa Sugoi.

Aidha, wananchi wamelalamikia kuwapo mkanganyiko kwa karatasi za kupigia kura katika kaunti ya Garissa Kaskazini Mashariki mwa Kenya, ambazo zilikutwa eneo la Chuka katikati mwa nchi hiyo huku za Kilifi zikipatikana katika kaunti jirani ya Mombasa katika eneo la Pwani.

Ofisa wa uchaguzi kaunti ya Kakamega, Joseph Ayatta, alithibitisha kuwa karatasi za kupigia kura kaunti ya Kirinyaga, zimepatikana katika kaunti ndogo ya Mumias Mashariki, magharibi mwa nchi. **BBC**

## Russia yashutumiwa kushambulia kiwanda cha nyuklia Ukraine

**Zaporizhzhia,** UKRAINE

UKRAINE imeishtumu kwa mara nyingine Russia kwa kushambulia kwa mabomu kituo kikubwa cha nishati ya nyuklia katika mji wa Zaporizhzhia na kudai kwamba Moscow imejihusisha katika ugaidi wa nyuklia.

Kiwanda hicho cha nyuklia cha serikali ya Ukraine kimesema wanajeshi wa Russia waliharibu mitambo mitatu ya mionzi kwenye kiwanda hicho katika shambulio la Jumamosi na kujeruhi mfanyakazi mmoja kwa kombora.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter "Ugaidi wa nyuklia wa Russia unahitaji jibu kali la Jumuiya ya Kimataifa, kuweka vikwazo kwenye sekta ya nyuklia ya Russia na mafuta ya nyuklia."

Kiwanda hicho kilichoko katika eneo linalodhibitiwa na Russia, kilishambuliwa pia Ijumaa, Moscow iliwashtumu wanajeshi wa Ukraine kwa mashambulizi hayo.

Russia ilikiteka kiwanda cha nyuklia cha Zaporizhzhia mapema mwezi Machi katika hatua za mwanzo za uvamizi wake dhidi ya Ukraine, lakini kiwanda hicho bado kinaendeshwa na mafundi wa Ukraine. **VOA**





Zilivyokuwa harakati za kampeni nchini Kenya. **PICHA: MTANDAO**

## Museveni: Sitaki mafuta ya Russia

**ENTEBE,** Uganda

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amesema nchi yake haitaagiza mafuta kutoka Russia kama alivyoomba Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergey Lavrov, wakati wa ziara yake ya hivi karibuni nchini Uganda.

Katika hotuba yake kwa taifa, Museveni amesema licha ya Russia kutaka kuiuzia Uganda mafuta kwa bei rahisi na bei ya mafuta kuongezeka sana, hayupo tayari kukubali ofa hiyo kwa sababu hataki kujiingiza katika mgogoro kati ya Marekani na Russia.

Alisema serikali yake itatafuta mbinu mbadala za kuhakikisha kwamba kuna mafuta ya kutosha nchini humo, wakati ikijitayarisha kutekeleza mikakati ya muda mrefu, ikiwa ni pamoja na kuwa na nishati safi, magari na pikipiki zinazotumia nguvu za umeme.

"Endapo tutanunua mafuta kwa bei rahisi kutoka Russia, ina maana kwamba tunakiuka vikwazo vya nchi za magharibi dhidi ya Russia. Tangu tatizo lilipoanza, nimekuwa nikiwasiliana na viongozi wa Russia na Marekani. Sasa mnaweza kuona mazungumzo yetu yameanza kuruhusu nafaka na ngano kusafirishwa kutoka Ukraine," alisema Museveni.



Museveni alisisitiza kwamba njia ya kusuluhisha uhaba wa bidhaa muhimu unaoshuhudiwa duniani kwa sasa ni kutumia diplomasia.

"Kama nataka kununua mafuta, ningeiambia Russia kusafirisha mafuta hayo hadi hapa na wangefanya hivyo. Lakini hatua hiyo inatuweka katika matatizo na Marekani ambayo sio jambo zuri. Kwa sasa, tutumie vizuri mafuta tuliyo nayo huku tukitafuta mbinu mbadala."

Rais Museveni ametoa msimamo huo siku chache baada ya kukutana na mabalozi wa ngazi ya juu wa Russia na Marekani.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergey Lavrov, alipokuwa Uganda Julai 26, mwaka huu, alisema kwamba Russia ilikuwa tayari kufanya mazungumzo na Uganda, kuhakikisha inapata mafuta ya bei rahisi au nafuu ili kukabiliana na uhaba wa bidhaa hiyo nchini humo.

"Tunauza mafuta kwa nchi zote ambazo zinataka na hakuna vizuizi vya aina yoyote kwa nchi yoyote inayotaka kununua mafuta, iwe India, taifa lolote la Afrika," alisema Lavrov.

Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, Linda Greenfield, alifanya mazungumzo na Rais Museveni nchini humo mwishoni mwa wiki na kumtahadharisha dhidi ya biashara ya mafuta na Russia. **VOA**

# NABI AIANDALIA 'SILAHA' SIMBA NGAO YA JAMII

**Na Saada Akida**

LICHA ya Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi kuhitaji muda zaidi wa kukiandaa kikosi chake, mwalimu huyo amesema anafanyia kazi ubora na madhaifu ya mpinzani wake, Simba kwa ajili ya mchezo wao wa Ngao ya Jamii.

**Yanga na Simba zitakaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/23 kwa kucheza mechi ya Ngao ya Jamii Agosti 13, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.**

Yanga hawakufanya vizuri katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Vipers ya Uganda kwenye kilele cha Siku ya Mwananchi iliyofanyika juzi Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Nabi alisema usajili wa mwaka huu ni mzuri, lakini kuna mambo madogo anayafanyia kazi na anaimani kikosi chake kitakuwa bora zaidi wakati huu akimulika mechi iliyoko mbele yao.

"Bado timu haijapata muunganiko kwa wachezaji wa msimu uliopita na wapya, tumecheza mechi ngumu ya kirafiki dhidi ya Vipers, imenipa mwanga wa kuona wapi natakiwa kufanyia kazi kabla ya mechi yetu ijayo ambayo ni muhimu kushinda ili kuanza kampeni yetu ya kutetea mataji yetu.

"Hata mimi nilitamani kupata ushindi kwenye mechi dhidi ya Vipers, lakini niseme tu mashabiki wasiwe na hofu, kuna mapungufu nimeyaona ya kufanyia kazi na kuimarisha ili kuwa bora zaidi," alisema Nabi.

Alisema ameona baadhi ya mapungufu na kwamba yote hayo yalitokana na uchache wa siku walizokaa kambini na wachezaji.

"Baadhi ya wachezaji wanafanya makosa, lakini inatokana na ukweli kwamba hawakufanya mazoezi kwa muda na niliwaongezea siku za kupumzika kwa sababu msimu uliopita ulikuwa mgumu sana," alisema Nabi.

Alisema anaendelea kufanyia kazi mapungufu hayo na ana imani, kikosi chake kitakuwa imara zaidi ya kutetea mataji yao matatu ikiwamo mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Simba.

Yanga baada ya kucheza mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba, watafungua rasmi kampeni yao ya kutetea taji la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Polisi Tanzania, mechi itakayopigwa Agosti 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha.

**MAELFU...**




Maelfu ya mashabiki wa Simba waliojitokeza katika Tamasha la Simba Day lililofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Prisons nayo yashusha 'maproo'*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kunusurika kushuka daraja msimu uliomalizika, Klabu ya Tanzania Prisons nayo imeamua kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi, ikiwa ni mara ya kwanza kwenye historia yake.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Shaaban Mtupa, amesema msimu huu wamesajili wachezaji watatu wa kigeni kutoka nchini Kenya.

Amemtaja mmoja wa wachezaji hao ni Amos Isense, kutoka Wazito FC ya Kenya ambaye amejiunga kwa mkataba wa miaka miwili, huku wengine wakitarajiwa kutangazwa wakati wowote ule taratibu zote zitakapokamilika.

"Zipo sura ngeni kwenye klabu, lakini si ngeni kwenye Ligi Kuu, pia kuna ngeni kabisa na zingine ni damu changa ambazo zina kiu ya mafanikio. Tuna wachezaji watatu hivi kutoka Kenya, mmoja ni huyo, tunaamini wataisaidia timu yetu kufanya vizuri. Wapo kila Mcha (Khamisi), Mlipili (Yusuph) na Mbisa (Mussa), hizi si sura ngeni kwenye ligi, lakini ni ngeni kwenye kikosi chetu, tumewasajili kwa ajili ya kuziba mapungufu yote ambayo sisi kama benchi la ufundi na kocha wangu Patrick Odhiambo tumeyaona," alisema Mtupa, straika wa zamani wa timu hiyo.

Alisema kuwa mpaka sasa wameacha wachezaji 10 na wamesajili wanane, huku usajili ukiwa unaendelea.

Mbali na Isense raia wa Kenya, Mlipili, Mbisa na Mcha, Prisons pia imewasajili Edwin Charlesa, Michael Masinda, na Ismail Mgunda Mtanzania aliyekuwa akicheza soka Afrika Kusini.

Prisons ni moja ya timu ambazo hazikufanya vyema msimu uliopita na kuponea kwenye mechi ya mwisho ya 'play off' dhidi ya JKT Tanzania.

Imeungana na timu ambazo zimekuwa hazina utamaduni wa kusajili wachezaji wa kigeni kama Mtibwa Sugar ambayo yenyewe tangu msimu uliopita ilianza kushusha 'maproo'

## Singida Big Stars yaipania Prisons

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Singida Big Stars, Mathias Lule, amesema wako fiti na imara kwa ajili ya kuanza mikakati yao ya kampeni yao ya kuleta ushindani mkubwa katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu mpya wa 2022/23.

Singida Big Stars itaanzia nyumbani katika mchezo wa kwanza wa ligi hiyo, dhidi ya Tanzania Prisons utakaopigwa Agosti 16, mwaka huu katika Uwanja wa Liti, Singida.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lule, alisema wamefanya usajili mzuri wa wachezaji kulingana na mahitaji ya timu yao ili kufanya vizuri zaidi kwa kutafuta ushindi katika michezo yote iliyopo mbele yao.

"Msimu huu utakuwa wa ushindani mkubwa, lakini kulingana na ubora wa kikosi chetu, nina imani kubwa ya kufanya vizuri zaidi katika michezo iliyopo mbele yetu ikiwamo mechi ya kwanza dhidi ya Tanzania Prisons," alisema Lule.

Alisema kulingana na usajili wa wachezaji uliofanyika, ni mzuri kutokana na kila nafasi kuwa na mchezaji zaidi ya wawili na kila mmoja kuonyesha kiwango kizuri na bora.

"Tunaanza kufungua pazia la ligi dhidi ya Tanzania Prisons, wako vizuri, tunahitaji kupata ushindi katika mchezo huo ambao tutacheza nyumbani," alisema Lule.

## Ruvu Shooting, KMKM zanukia fainali Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU za Ruvu Shooting na KMKM zina nafasi ya kutinga fainali ya Mashindano ya Maandalizi ya msimu mpya ('Pre-season Tournament'), endapo zitashinda michezo yao ya marejeano ambao itakayopigwa leo katika Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Katika michuano hiyo iliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ruvu Shooting itavaana na Kipanga leo majira ya saa 10 alasiri, wakati Kundemba watavaana na KMKM majira ya Saa 1:00 usiku.

Ruvu shooting katika mchezo wake wa nyumbani iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wanajeshi wa Kipanga, wakati KMKM wenyewe walipata ushindi mwembamba wa bao 1-0 dhidi ya Kundemba FC.

Kwa matokeo hayo timu za Ruvu Shooting na KMKM zinapaswa kupata ushindi ama sare ili zitinge hatua ya fainali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Ali Bakar alisema hatua ya fainali itachezwa keshokutwa, Alhamisi huku na kwamba muda utapangwa baada ya kukamilika michezo ya mwisho ya marudiano.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ODOI AWINDWA LEICESTER



KLABU za Leicester na Southampton zinamwania winga, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 21 baada ya nyota huyo kuomba kuondoka Chelsea kwa mkopo kabla ya dirisha la usajili kufungwa. ***(Guardian)***

### DORTMUND YATUA CHELSEA

KLABU ya Borussia Dortmund ya Ujerumani pia ina nia ya kutaka kumnunua mchezaji Callum Hudson-Odoi wa Chelsea mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### SESKO AWANIWA UNITED


MANCHESTER United inaendelea kumsaka mshambuliaji wa Slovenia mwenye umri wa miaka 19, Benjamin Sesko kutoka Red Bull Salzburg. ***(Express)***



### WERNER KUREJEA LEIPZIG

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 26, anakaribia kurejea RB Leipzig. ***(Mail)***

### CELSO KUFUNGWA VILLARREAL



KLABU ya Villarreal ina uhakika wa kumchukua kiungo wa kati wa Argentina, Giovani lo Celso mwenye umri wa miaka 26, kutoka Tottenham kwa mkataba wa kudumu baada ya kufanikiwa kwa mkopo msimu uliopita. ***(Fabrizio Romano)***

### BAYERN YAIPOTEZEA UNITED

MKURUGENZI wa Soka wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic amepuuza mapendekezo kwamba, Manchester United imefanya uchunguzi kwa ajili ya mchezaji wa kimataifa wa Ujerumani, Leroy Sane mwenye umri wa miaka 26. ***(Manchester Evening News)***


### NEWCASTLE NAYO HAIPITWI

KLABU ya Newcastle pia ipo tayari kumsajili Benjamin Sesko ambaye anatajwa kuwa bora sana. ***(Northern Echo)***

### WOLVES YAMGOMEA GOMES

KLABU ya Wolves imekataa ofa ya mkopo kutoka kwa klabu ya Italia ambayo haijatajwa jina kwa ajili ya mlinzi wao Mreno, Toti Gomes mwenye umri wa miaka 23. ***(Express and Star)***

### SANGARE AJIFUNGA PSV




KIUNGO wa kati wa Ivory Coast, Ibrahim Sangare mwenye umri wa miaka 24, ameongeza mkataba wake na PSV Eindhoven hadi mwaka 2027, licha ya West Ham kumtaka. ***(Sun)***

### SENESI KUTUA BOURNEMOUTH

MLINZI wa Argentina, Marcos Senesi mwenye umri wa miaka 25, anatarajiwa kuhamia Bournemouth kutoka Feyenoord kwa pauni milioni 12.6. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# GUARDIOLA: HAALAND KAANZA KAMA MESSI

**MANCHESTER,** England

**Wafungaji bora hawatosheki, huwa na njaa na wanataka zaidi, akifunga mawili anataka matatu...**

PEP Guardiola amesema njaa ya mabao ya Erling Haaland inamkumbusha wakati wake wa kufanya kazi na Lionel Messi baada ya raia huyo wa Norway kufungua akaunti yake ya mabao pale Manchester City, Jumapili.

**Haaland aliyetua hapo msimu huu wa majira ya joto alifunga mabao yote mawili katika ushindi wa 2-0 wa City dhidi ya West Ham huku mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England wakianza vema msimu wao mpya wa 2022-23.**

Lakini katika mahojiano na Sky Sports baada ya mchezo huo, Haaland alidokeza kuwa hakufurahi kutofunga hat-trick, kama alivyofanya kwenye mechi yake ya kwanza katika klabu iliyopita ya Borussia Dortmund dhidi ya Augsburg, Januari 2020.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari baada ya ushindi huo dhidi ya 'Wagonga Nyundo' hao wa London, Guardiola alisifu 'njaa' ya mshambuliaji wake mpya na kumfananisha na gwiji wa zamani wa Barcelona, Messi, akisema: "Hiyo ni nzuri, naipenda.

"Nilikuwa na bahati kama kocha kuwa na Messi na alipofunga mawili, alitaka matatu, na alipofunga matatu, alitaka manne.

"Wafungaji bora hawatosheki, huwa na njaa na wanataka zaidi."

Haaland alikosolewa baada ya kukosa nafasi kadhaa wakati City ikifungwa 3-1 na Liverpool kwenye Ngao ya Jamii wiki iliyopita na Guardiola alifurahishwa na majibu yake Jumapili.

Alishinda na kufunga penalti katika kipindi cha kwanza, kabla ya kukimbilia pasi ya Kevin De Bruyne na kupachika bao la pili na kuwawezesha kuondoka na pointi zote tatu.

"Ninajua jinsi alivyokabiliana na ukosoaji mwingi wiki hii," alisema Guardiola.

"Alikuwa mtulivu sana, alifanya mazoezi vizuri sana, lakini kwa jinsi alivyopiga mpira kwa penalti, nilisema 'napenda'."


SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
MIDTJYLLAND
VERSUS
BENFICA
1 | 4.29
X | 3.84
2 | 1.71

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG AKATAA KUWALAUMU MABEKI



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik Ten Hag, alisisitiza kwamba, hawezi kuwalaumu mabeki kwa kufungwa bao 2-1 na Brighton kwenye mchezo wa Ligi Kuu England pale Old Trafford, Jumapili.

Brighton walijikuta wakiwa mbele kwa mabao 2-0 hadi mapumziko baada ya Pascal Gross kufunga mabao mawili kipindi cha kwanza.

Ten Hag aliamua kumwacha Cristiano Ronaldo kwenye benchi kutokana na kukosa utimamu wa mwili, lakini alimwingiza katika kipindi cha pili, wakati wakipata bao la kufutia machozi kutoka kwa Alexis Mac.

Brighton walipata ushindi wao wa kwanza ugenini katika Uwanja wa Old Trafford.

Hata hivyo, bosi huyo wa zamani wa Ajax alikataa kulaumu safu yake ya ulinzi kwa kushindwa, akiwaambia waandishi wa habari: "Haikuwa ulinzi. Tunalinda kama timu na tulifanya makosa ya pasi ambayo hayakuwa ya lazima kwenye safu ya kati, kisha wakachukua nafasi.

"Lazima tuwe bora kwenye muunganiko kwa sababu tumeshaweka na wanatakiwa wafanye kazi tuliyozungumza ambayo wameteuliwa, sivyo tulivyofanya halafu tukaadhibiwa."



## Deschamps anaamini Pogba atacheza Kombe la Dunia

**PARIS,** Ufaransa

DIDIER Deschamps bado ana imani Paul Pogba atakuwa fiti kuichezea Ufaransa kwenye michuno ya Kombe la Dunia licha ya kukosa mwanzo wa msimu huu kutokana na majeraha.

Pogba alipata tatizo la goti katika maandalizi ya msimu mpya baada ya kurejea Juventus kutoka Manchester United kwa uhamisho wa bure.

Kulikuwa na mapendekezo ya awali ya upasuaji ambayo yangeweza kumfanya mshindi huyo wa Kombe la Dunia kukosa michuano ya kule Qatar baadaye mwaka huu, lakini amechagua matibabu ambayo yanalenga kuhakikisha kurudi kwa haraka.

Pogba anatazamiwa kupangwa tena na N'Golo Kante katika safu ya kiungo ya Ufaransa Novemba, ingawa mchezaji huyo wa Chelsea amekuwa akisumbuliwa na majeraha katika misimu ya hivi karibuni.

"Tunazungumza kuhusu wachezaji ambao wanahitajika sana - wachezaji wawili ambao wana uzoefu mku[...] wa na viongozi," alisen[...] Deschamps akiiambia Le P[...] risien juu ya wachezaji ha[...] wawili.

"Ni muhimu wawepo, lal[...] ni sisi kamwe hatuko salam[...] Ninawasiliana na Paul. Us[...] iriki wake katika Kombe [...] Dunia ni muhimu."

Antoine Griezmann [...] mchezaji mwingine amba[...] bado anaonekana kuw[...] muhimu kwa mipango y[...] Deschamps, licha ya k[...] funga mabao matatu pek[...] kwenye LaLiga msimu uli[...] pita.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# AZAM YAWASILI KUIVAA ZESCO KATIKA 'AZAMKA'

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Azam FC kilichokuwa nchini Misri kwenye mji wa El Gouna, kilitarajiwa kuwasili nchini jana baada ya kumaliza kambi yake ya zaidi ya wiki mbili kujiandaa na msimu mpya wa mashindano, huku kikitarajia kucheza dhidi ya Zesco Jumapili wiki hii kwenye siku maalumu ya kuwatambulisha wachezaji wapya wa timu hiyo, ikiitwa 'Azamka'.

Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Abdihamid Moalin, amesema baada ya kambi nchini Misri ameangalia wachezaji wake wote na kuwafahamu na ana furaha sana kwa usajili uliofanyika, kwani ni wa wachezaji wengi vijana wenye nguvu na kasi.

"Nina furaha ya usajili wa wachezaji wengi ambao ni vijana ambao wamekuja kutuongezea kasi na nguvu, nina uhakika msimu unaoanza tutafanya vizuri," alisema kocha huyo.

**Kuhusu kambi, alisema ameridhishwa na kambi na mazoezi aliowapa vijana wake, hivyo kwa sasa anachotaka ni kukiangalia kile alichokifanya kwenye uwanja wa soka.**

Ikiwa nchini humo, Azam ilicheza michezo miwili ya kirafiki, mechi yake ya kwanza ikicheza dhidi ya Wadi Degla na kuchapwa bao 1-0, ya pili ikishinda bao 1-0 dhidi ya Grand FC, bao lililofungwa na Prince Dube.

Timu hiyo itacheza mechi yake ya kwanza Jumapili mara baada ya kutua dhidi ya Zesco ya Zambia.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imesema kuwa mechi hiyo itakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, itakuwa ni maalumu kwa ajili ya kilele cha siku yao walioipa jina la 'Azamka', ambayo ni maalumu kwa kuwatambulisha wachezaji wa zamani na wapya watakayoichezea timu hiyo msimu mpya wa mashindano ya ndani na kimataifa.




Watoto wa halaiki wakitoa burudani katika Tamasha la Simba Day lililofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



# Dida atimka Mbeya City

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mbeya City imetangaza rasmi kuachana na wachezaji tisa ambao hawatokuwa nao msimu ujao wa mashindano mbalimbali ambayo itashiriki, akiwamo kipa mkongwe, Deogratius Munishi 'Dida.'

Ofisa Mtendaji, Mkuu wa klabu hiyo, Emmanuel Kimbe, amesema wachezaji hao wameachwa kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kumaliza mikataba yao ndani ya klabu hiyo na wengine kuvunja.

"Tunawatakiwa kila la kheri wanakokwenda kuendeleza maisha yao ya soka, lakini tunawashukuru kwa mchango mkubwa waliotoa wakati wote wa utumishi wao uliotukuka ndani ya klabu yetu," alisema Kimbe.

Alisema kwa sasa klabu inaendelea na harakati za usajili kwa ajili ya kutengeneza kikosi imara kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mbali na kipa aliyefanya vyema sana msimu uliopita hasa aliposimama langoni dhidi ya timu vigogo vya Simba na Yanga, 'Dida', hawatokuwa pia na nahodha wao Mpoki Mwakenyuke.

Wengine ni Herbert Lukindo, Siraji Juma, Peter Mapunda, Edgar Mbembela, Selemani Ibrahim, Babilas Chitembe na Patson Shigala.

Dida amewahi kuzidakia timu za Simba ambayo aliichezea mara mbili kwa vipindi tofauti, pia ana rekodi ya kuzidakia timu zote tatu kubwa nchini, Simba, Yanga na Azam FC.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 09/08/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:15 | 1040 | Sabah vs Sarawak | 1.51 | 4.20 | 5.60 |
| 16:00 | 2530 | Negeri Sembilan vs Penang | 1.71 | 3.74 | 4.03 |
| 17:30 | 1646 | Umm-Salal SC vs Al Sadd SC | 3.09 | 4.12 | 1.87 |
| 18:00 | 2098 | Moroka Swallows FC vs Cape Town City | 3.20 | 2.90 | 2.37 |
| 19:00 | 3622 | Zalgiris vs Bodo Glimt | 4.31 | 3.61 | 1.75 |
| 19:00 | 4391 | Gzira United vs Wolfsberger AC | 5.68 | 4.16 | 1.53 |
| 19:30 | 3153 | Ghazl EL Mahallah vs Pyramids | 6.04 | 3.42 | 1.62 |
| 20:00 | 2508 | Viktoria Plzen vs Sheriff Tiraspol | 1.51 | 3.90 | 6.20 |
| 20:00 | 3103 | Norrby IF vs IK Brage | 2.04 | 3.51 | 3.51 |
| 20:00 | 3483 | Pyunik Yerevan vs Red Star Belgrade | 7.60 | 4.80 | 1.35 |
| 20:00 | 4475 | Apollon Limassol vs Maccabi Haifa | 3.26 | 3.26 | 2.15 |
| 20:30 | 2594 | Kaizer Chiefs vs Maritzburg Utd | 1.81 | 3.16 | 4.71 |
| 20:45 | 2841 | Midtjylland vs Benfica | 4.29 | 3.84 | 1.71 |
| 21:00 | 3065 | B36 Torshavn vs Viborg FF | 7.07 | 4.75 | 1.39 |
| 21:00 | 4082 | Dinamo Zagreb vs Ludogorets Razgrad | 1.65 | 3.79 | 4.79 |
| 21:00 | 5048 | Ferencvaros TC vs Karabakh | 2.17 | 3.25 | 3.20 |
| 21:30 | 2348 | Sturm Graz vs Dynamo Kiev | 2.28 | 3.19 | 3.04 |
| 21:30 | 3100 | Wisla Krakow vs GKS Katowice | 1.70 | 3.58 | 4.32 |
| 21:30 | 3470 | Shrewsbury vs Carlisle | 1.62 | 3.77 | 5.22 |
| 21:30 | 5230 | PSV Eindhoven vs Monaco | 2.22 | 3.50 | 2.90 |
| 21:45 | 1117 | Accrington vs Tranmere | 2.05 | 3.46 | 3.36 |
| 21:45 | 1214 | Walsall vs Swindon Town | 2.56 | 3.31 | 2.61 |
| 21:45 | 1447 | AFC Wimbledon vs Gillingham | 2.27 | 3.31 | 3.01 |
| 21:45 | 1484 | Rangers vs Union Saint Gilloise | 1.76 | 3.58 | 4.28 |
| 21:45 | 1634 | Crawley Town vs Bristol Rovers | 3.01 | 3.41 | 2.23 |
| 21:45 | 1677 | Cheltenham vs Exeter | 2.57 | 3.28 | 2.62 |
| 21:45 | 1860 | Grimsby vs Crewe | 2.41 | 3.42 | 2.72 |
| 21:45 | 1928 | Fleetwood Town vs Wigan | 3.82 | 3.42 | 1.92 |
| 21:45 | 2190 | Northampton vs Wycombe | 3.10 | 3.15 | 2.30 |
| 21:45 | 2388 | Luton Town vs Newport | 1.53 | 4.12 | 5.63 |
| 21:45 | 2660 | Doncaster vs Lincoln | 2.62 | 3.38 | 2.52 |
| 21:45 | 2831 | Bolton vs Salford City | 1.83 | 3.57 | 4.02 |
| 21:45 | 2962 | Ipswich vs Colchester | 1.40 | 4.52 | 7.24 |
| 21:45 | 2968 | Bradford City vs Hull City | 3.01 | 3.36 | 2.25 |
| 21:45 | 3320 | Harrogate vs Stockport | 3.32 | 3.57 | 2.02 |
| 21:45 | 3640 | Forest Green vs Leyton Orient | 1.88 | 3.47 | 3.92 |
| 21:45 | 4219 | Rochdale vs Burton | 2.46 | 3.33 | 2.72 |
| 21:45 | 4527 | Norwich City vs Birmingham | 1.66 | 3.82 | 4.73 |
| 21:45 | 4716 | MK Dons vs Sutton United | 1.71 | 3.61 | 4.72 |
| 21:45 | 4949 | Oxford Utd vs Swansea | 2.86 | 3.41 | 2.32 |
| 21:45 | 5094 | Cardiff vs Portsmouth | 2.11 | 3.36 | 3.31 |
| 21:45 | 5117 | Huddersfield vs Preston | 2.51 | 3.11 | 2.81 |
| 21:45 | 5270 | Blackpool vs Barrow | 1.40 | 4.62 | 6.82 |
| 21:45 | 5630 | Mansfield vs Derby | 2.76 | 3.31 | 2.44 |
| 21:45 | 5747 | Morecambe vs Stoke City | 4.23 | 3.57 | 1.79 |
| 21:45 | 5851 | Charlton vs QPR | 2.87 | 3.37 | 2.33 |
| 22:00 | 1295 | National Bank vs Farco FC | 2.20 | 2.85 | 3.70 |
| 22:00 | 2099 | Zamalek vs Misr Lel Makasa | 1.17 | 6.43 | 16.09 |
| 22:00 | 3667 | Reading vs Stevenage | 1.60 | 3.86 | 5.21 |
| 22:00 | 4164 | Shkupi Skopje vs Shamrock Rovers | 2.34 | 3.38 | 2.88 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Nipashe

Jumanne Agosti 9, 2022




Nabi aiandalia 'silaha' Simba Ngao ya Jamii UKURASA 20




Wachezaji wa Simba na benchi la ufundi la timu hiyo kuelekea msimu mpya wa 2022/23, waliotambulishwa jana katika Tamasha la Simba Day lililofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba day babkubwa

## ●●● Yavunja rekodi zake, kila kitu usipime, usajili mpya waanza kulipa, Okwa afanya...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeonyesha kwamba wao ndio waasisi halisi wa tamasha kubwa la kutambulisha wachezaji kuelekea msimu mpya hapa nchini baada ya jana kuja kivingine na kukosha nyoyo si tu za mashabiki wao bali wapenzi wote wa soka ndani na nje ya nchi.

Katika tamasha hilo maarufu kama Dimba Day, ambalo ni la 14 kwa Simba tangu liasisiwe na aliyekuwa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Dalali, mwaka huu lilifana zaidi na kukonga nyoyo za mashabiki wa soka ambapo pia walifurahia burudani ya kandanda safi kwa timu yao kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya mabingwa wa Ethiopia, Saint George SC.

Simba imekuwa ikitumia tamasha hilo kutambulisha wachezaji wao wa msimu mpya, jezi na kuuza vifaa vingine vya michezo za klabu hiyo, na kila mwaka wamekuwa wakiliboresha zaidi kwa burudani na mambo mengine mengi ya kuburudisha.

**MECHI**

Mabao ya Simba katika mechi hiyo yalifungwa na Denis Kibu na Nelson Okwa aliyesajiliwa msimu huu kutoka Rivers United ya Nigeria

Mechi ilianza kwa timu kucheza kati zaidi na ilionekana ni kama zinasomana, lakini zilianza kubadilika kadri muda ulivyozidi kusonga mbele.

Kuanzia dakika ya 16 ndipo kulipoanza kuwa na matukio muhimu, kwani Simba kwa mara ya kwanza ilifika langoni mwa wapinzani wao kwa krosi ya Israel Mwenda kukosa muunganishaji kabla ya mabeki wa Saint George kuokoa.

Dakika ya 18 ya mchezo, pasi ya Augustine Okra, ilimkuta Mohamed Hussein, ambaye alipenyeza mpira kwa Habib Kyombo kisha alianguka, lakini ulifika kwa Kibu aliyeachia shuti kali lililokwenda moja kwa moja wavuni.

Beki mpya wa Simba, Mohamed Quattara raia wa Ivory Coast aliyesajiliwa msimu huu kutoka Al-Hilal, alifanya kazi ya ziada kuondoka mpira mara mbili kwenye msitari wa goli iliyopigwa na wachezaji Ismail Ouro-Agoro na Beneyam Belay wa St George baada ya kutokea shambulizi kali langoni.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, lakini ni Simba ilipachika tena bao la pili kupitia kwa Okwa.

Ilikuwa ni kazi kubwa iliyofanya na yeye mwenyewe, akimega pande kwa Pape Sakho aliyepiga shuti lililowababatiza mabeki wa St George, kabla ya kumfikia Chama kwenye wingi ya kushoto aliyewafinya mabeki wakaanguka na kupiga krosi iliyomfikia mfungaji, akaujaza wavuni na kuifanya Simba kuondoka na mabao 2-0.

**UWANJA WATAPIKA**

Wanachama na mashabiki wa Simba waliujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa mapema huku klabu hiyo ikitangaza kumaliza kuuza tiketi zote saa 7:00 mchana, na kuvunja rekodi ya msimu uliopita ilipomaliza tiketi zote saa 7:10 mchana.

Wasanii mbalimbali, wakiongozwa na Zuchu 'waliwachizisha' mashabiki wake, ambao muda wote walionekana kufurahi wakipunga bendera nyeupe na nyekundu.

Mapema tu majira ya saa 8:42 majukwaa yote ya Uwanja wa Benjamin Mkapa yalikuwa yamejaa huku nderemo za kelele za mashabiki zikiendelea kurindima uwanjani. Ukiachilia mbali burudani za muziki ndani zikipambwa na wasanii mbalimbali, nje ya uwanja ilikuwa ni balaa kwa mashabiki wa Simba kujikusanya makundi kwa makundi na kupiga vigoma na kucheza.

**ALEX SONG, KALOU NDANI**

Kiungo wa zamani wa Arsenal, Alex Song na winga wa zamani wa Chelsea, Salomon Kalou, walikuwa ni miongoni mwa wageni waalikwa katika tamasha hilo huku Bondia wa Ngumi za Kulipwa Tanzania, Shaban Kaoneka, ambaye hivi majuzi alimtwanga Karim Mandonga, naye alitambulishwa kuwa ni 'Mnyama'.

**KAGERE, LWANGA HESHIMA**

Katika hatua nyingine Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally aliwaita wachezaji wawili wa kimataifa, Meddie Kagere na Taddeo Lwanga kwa ajili ya kuagwa kwa heshima na mashabiki wa soka katika tamasha hilo.

**KIKOSI CHA NYOTA 28**

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed aliwatambulisha wachezaji 28, 21 wa zamani, saba wapya kati yao watano wakiwa wakigeni na wawili wazawa.

Wachezaji hao ni Ally Salim, Feruz Ahmed, Gadiel Michael, Jonas Mkude, Israel Mwenda, Peter Banda, Shomari Kapombe, Sadio Kanoute, Joash Onyango, Pape Sakho na Erasto Nyoni, Mzamiru Yassin, Jimson Mwanuke, John Bocco, Aishi Manula, Kennedy, Juma, Benno Kakolanya, Enock Inonga, Kibu Denis, Mohamed Hussein na Clatous Chama. Wachezaji wa kigeni ni Mohamed Quattara, Victor Akpan, Augustine Okrah, Moses Phiri na Dejan Georgijevic, huku wazawa wakiwa ni Nassor Kapama na Habib Kyombo.

**SIMBA QUEENS YASHINDA**

Awali, timu ya Wanawake cha Simba, Simba Queens, kilicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Fountain Gate na kuibuka na ushindi wa mabao 2-0.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >